KUTATHMINI NAFASI YA MWANAMKE KATIKA MASHAIRI YA KISWAHILI: UCHUNGUZI WA MASHAIRI YA SHAABAN ROBERT NA MATHIAS MNYAMPALA

ALI EDRIS ALI

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2014

UTHIBITISHI

Mimi **Profesa T.S.Y.M.Sengo** ninathibitisha kuwa nimesoma tasinifu hii iitwayo ***Kutathmini Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala*** na ninapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya M.A. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

_____

Sheikh, Daktari, Professa T.S.Y.M. SENGO

(Msimamizi)

_____

Tarehe

HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi **Ali Edris Ali**, ninathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

……..

Sahihi

……..

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa Wananchi wote wa Libya ambao hivi sasa wapo katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yanayosababisha mauaji ya raia wasio na hatia. Kwa kazi hii ninawaomba wasitishe mapigano na warejeshe amani kama ilivyokuwa zamani. Pia niaitabaruku kazi hii kwa mke wangu na mtoto wetu Aisha Ali Edris Ali na kuwahusia kuwa wafanye jitihada katika kusoma ili wapate kufika katia ngazi ya elimu niliyoifikia mimi na hata kunizidi Inshaallah.

SHUKURANI

Hakuna apasae kushukuriwa wa kwanza katika mafanikio yoyote ya mwanadamu isipokuwa Mwenyezi Mungu Subhana Wataala. Hivyo, shukurani zangu za kwanza napenda kuzitoa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema katika kipindi chote nilichokuwa ninaandika kazi hii. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia familia yangu salama na amani katika kipindi hiki ambapo nchi yangu ya Libya ipo katika machafuko ya mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Kwa hili, ninasema **Alhamdulillah Rabi Laalamina**.

Shukurani zangu za pili nazitoa kwa msimamizi wangu Sheikh, Daktari, Profesa T. S. Y. M. SENGO kwa maongozi mema katika kipindi chote cha uandishi wa tasinifu yangu. Msimamizi huyu ni hodari wa kusahihisha kazi kwa kusoma neno kwa nno na ni jambo la kawaida kukuta wino mwekundu unaozidi maandishi ya mtafiti katika kila ukurasa wa kazi aliyoisahihisha. Kwa mara ya kwanza kukutana na hali hiyo, nilikata tamaa na kudhani kwamba sitaweza kufuzu masomo yangu. Kwa bahati nzuri, msimamizi wangu alinitia moyo kuwa nisiakate tamaa kwani huko ndiko kujifunza na shule ndivyo ilivyo. Kutokana na ushauri huo niliongeza jitihada katika masomo na leo hii nimefikia hatua hii.

Shukurani zangu za tatu nazitoa kwa familia yangu iliyopo katika mji wa Sebha nchini Libya kwa kunisaidia kifedha na ushauri katika kipindi chote cha masomo yangu. Mimi ninalipiwa gharama za masomo na Serikali ya Libya kwa asilimia mia moja. Kutokana na machafuko na vita vinavyoendelea katika nchi yangu imekuwa ni vigumu kwa serikali kutupatia fedha kwa wakati na wakati mwingine kutopatiwa kabisa. Kwa hali hiyo, familia yangu imekuwa ikinitumia fedha mara kwa mara na

kunifanya nisiishi kwa shida sana hapa Tanzania. Ninasema asante sana kwa familia yangu.

Shukurani zangu za nne ninazitoa kwa mke wangu mpenzi ambaye kwa sasa nipo naye hapa Tanzania. Mke wangu amekuwa akinitia moyo kwamba siku moja nitafanikiwa na kukamilisha kazi yangu. Leo hii ninafurahi kuona hamasa na moyo aliyokuwa akinitia vimenisaidia kukamilisha kazi yangu. Ninakushukuru sana mke wangu kwa mawazo, uvumilivu na muongozo wako na Mwenyezi Mungu ndiye atakayekulipa. Pia, ninapenda kumshukuru mtoto wetu Aisha Ali Edris Ali kwa kunielewa kila mara nilipomfukuza asinisumbue wakati ninaandika kazi yangu.

Salamu zangu za tano ninazitoa kwa Walimu wote wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kunifundisha na kunipatia miongozo mbalimbali ya kukamilisha kazi yangu. Miongoni mwao ni Profesa Emmanuel Mbogo, Daktari Anna Kishe, Daktari Peter Pembe Lipembe, Daktari Hanna Simpassa, Daktari Zelda Elisifa na Hadija Jilala. Ninasema asanteni sana walimu wangu kwa kunifundisha lugha ya Kiswahili ambayo kwa sasa ninaiweza kiasi ikilinganishwa na nilivyokuja kutoka Libya kwa mara ya kwanza.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni “Kutathmini Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Kiswahili: *Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala*.” Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kulinganisha nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ili kubaini falsafa yao juu ya mwanamke katika jamii. Madhumuni mahususi ya utafiti huu yalikuwa ni kulinganisha na kulinganua usawiri wa mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala, kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha ya kisanaa inayotumiwa na Shaaban Robert na Mathias Mnyampala katika kusawiri nafasi ya mwanamke na kubainisha falsafa ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala juu ya nafasi waliyompa mwanamke katika mashairi yao. Nadharia ya Kifeministi ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Mbinu za usaili, hojaji na usomaji makini ndizo zilizotumika katika kukusanya data za utafiti.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mwanamke anasawiriwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume, mwanamke ni kiumbe mpole na mnyenyekevu kwa mumewe, ni mama na mlezi katika jamii, mwanamke na suala la uaminifu na mwanamke na suala la umalaya na uasherati. Matumizi ya lugha ya tamathali za takriri, tashibiha, taswira na ishara ndizo zilizotumika kusawiri nafasi ya mwanamke katika mashairi yaliyotafitiwa. Falsafa yao juu ya mwanamke inasema, mwanamke ni kiumbe mwenye daraja ya juu katika malezi na ustawi wa jamii nzima na si familiya yake tu.

YALIYOMO

Uthibitishi ii

Haki Miliki iii

Tamko…. iv

Tabaruku v

Shukurani vi

Ikisiri……. viii

Yaliyomo ix

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI……. 1

1.0 Usuli wa Tatizo la Utafiti 1

1.1 Tatizo la Utafiti 4

1.2 Malengo ya Utafiti 5

1.2.1 Lengo Kuu la Utafiti 5

1.2.2 Malengo Mahususi 5

1.2.3 Maswali ya Utafiti 6

1.3 Umuhimu wa Utafiti 6

1.4 Mipaka ya Utafiti 7

1.5 Matatizo ya Utafiti na Utatuzi Wake 8

1.6 Hitimishi 8

SURA YA PILI: UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ……. 9

2.0 Utangulizi 9

2.1 Ushairi wa Shaaban Robert 9

2.2 Ushairi wa Mathias Mnyampala 15

2.3 Mkabala wa Kinadharia 17

2.3.1 Nadharia ya Ufeministi 17

2.4 Hitimishi 19

SURA YA TATU: NJIA ZA UTAFITI 21

3.0 Eneo la Utafiti 21

3.1 Kundi Lengwa 21

3.2 Sampuli ya Utafiti 22

3.3 Mbinu za Kukusanyia Data 23

3.3.1 Mbinu ya Usaili 23

3.3.2 Hojaji 23

3.3.3 Mbinu ya Usomaji Makini 24

3.4 Mbinu ya Uchambuzi wa Data 24

3.5 Kuaminika kwa Data za Utafiti 26

3.6 Usahihi wa Data za Utafiti 26

3.7 Hitimisho 26

SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 28

4.0 Utangulizi 28

4.1 Usawiri wa Mwanamke katika Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala 28

4.1.1 Mwanamke kama Chombo cha Starehe 29

4.1.2 Mwanamke ni Mpole, Mnyenyekevu kwa Mwanaume 32

4.1.3 Mama na Malezi katika Jamii 38

4.1.4 Mwanamke na Suala la Uaminifu 41

4.1.5 Suala la Uasherati na Umalaya katika jamii 45

4.2 Matumizi ya lugha ya Kisanaa katika Mashairi ya Washairi Teule 47

4.2.1 Matumizi ya Takriri katika Mashairi ya Washairi teule 48

4.2.2 Matumizi ya Tashibiha katika Mashairi ya Washairi Teule 51

4.2.3 Matumizi ya Taswira katika Mashairi ya Washairi Teule 54

4.2.4 Ishara katika Mashairi ya Washairi Teule 57

4.3 Falsafa ya Washairi Teule Juu ya Mwanamke..... 60

4.3.1 Falsafa ya Shaaban Robert juu ya Mwanamke 60

4.3.2 Falsafa ya Mathias Mnyampala juu ya Mwanamke 64

4.3.3 Hitimisho..... 65

SURA TA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 68

5.0 Utangulizi..... 68

5.1 Muhtasari wa Sura za Tasinifu 68

5.2 Hitimisho..... 70

5.2.1 Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Washairi Teule..... 70

5.2.2 Matumizi ya lugha ya Kisanaa katika Mashairi ya Washairi Teule 71

5.2.3 Falsafa ya Washairi Wateule juu ya Mwanamke..... 72

5.3 Mapendekezo 73

MAREJELEO 74

VIAMBATANISHO 80

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Shaaban Robert ni mwandishi mwenye jina kubwa katika uandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili ambaye mpaka leo bado hajapata mtu wa badali katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Njogu na Chimeraha, 1999). Hii ina maana kwamba, hakuna mtunzi wa kazi za fasihi ambaye ameweza kumfikia Shaaban Robert katika utunzi wake (Chuachua, 2011). Walibora (2013) anawataja akina Wamitila na Kezilahabi kuwa ni miongoni mwa watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi lakini bado hawajaweza kumfikia Shaaban Robert. Anaendelea kueleza kwamba, si tu hawajamfikia kwa idadi ya kazi alizoandika lakini pia hawajamfikia kwa ujuzi wa kisanaa hasa katika utumizi wa lugha na hasa kipengele cha uteuzi wa maneno au msamiati anaoutumia katika kazi zake za mashairi, riwaya pamoja na insha. Kutokana na umahiri wake –Shaaban Robert, katika utunzi wa kazi za fasihi, watafiti mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wamevutiwa katika kuhakiki na kutafiti kuhusu kazi zake. Kwa hakika Shaaban Robert ni nguli wa utunzi katika fasihi ya Kiswahili aliyeandika kazi zaidi ya 25 zikiwemo riwaya, mashairi na Insha (Kezilahabi, 1983). Naye Twaib (2009) anaeleza kwamba, si kwamba hakuna mtunzi wa fasihi ya Kiswahili aliyeweza kuandika kama Shaaban Robert kwa maana ya idadi ya kazi pekee bali hakuna aliyemfikia kwa utaalamu wa kutumia lugha katika kuandika kazi zake. Shaaban Robert alikuwa mtu mahiri katika utumizi wa lugha, kiasi kwamba kila asomaye kazi zake huvutiwa sana na lugha nzuri ya Kiswahili iliyotumika katika riwaya, ushairi na insha (Momanyi, 2001).

Chuachua (2011) anaeleza kwamba, Shaaban Robert hakuwa mtaalamu wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha wake peke yake bali pia aliweza kubuni mandhari isiyo halisi na kuitumia kuwasilishia mambo mbalimbali yanayotokea katika mandhari halisi. Mfano mzuri wa kuunga mkono hoja hii unapatikana katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Anaendelea kueleza kwamba, kutokana na matumizi haya ya mandhari isiyo halisi Shaaban Robert ameweza kuwasilisha na kuzungumzia masuala mbalimbali ambayo yanaigusa jamii nzima na si ile ya Kitanzania peke yake. Kezilahabi (1976a) anaeleza kwamba, unaposoma riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* utaona kwamba, mambo yanayoelezwa katika riwaya hiyo yanatokea katika maeneo mbalimbali ya nchi za Afrika na popote pale duniani ambapo kuna unyonyaji na utawala usio wa haki na sheria. Hii inatokana na mbinu za kisanaa alizotumia katika utunzi wa riwaya hizo kuwa ni za hali ya juu mno kiasi cha kuweza kuakisi mambo ambayo yanafanyika na kutendeka katika nchi mbalimbali duniani. Mawazo ambayo yanapatikana katika riwaya zake zilizotajwa na Kezilahabi (1976a) yanapatikana pia katika kazi zake za mashairi za *Ashiki Kitabu Hiki* na *Pambo la Lugha*.

Shaaban Robert alikuwa si mtunzi tu wa kazi za fasihi bali pia alikuwa mwalimu kwa wanafasihi wengi ambao walimuiga katika kutunga mashairi na kazi nyingine fasihi. Kwa mfano, Mathias Mnyampala ni miongoni mwa watunzi wa ushairi wa Kiswahili ambaye kwa maneno yake mwenyewe anakiri kwamba, alijifunza kutoka kwa Shaaban Robert kutunga mashairi aliyopata kuyatunga katika *Waadhi wa Ushairi, Ngonjera za UKUTA* na mengineyo (Abdullazizi, 1969). Mnyampala ni bingwa katika utunzi wa mashairi yenye kufuata urari wa vina na mizani huku

akitumia lugha tamu kwa ulimi wa kuitamka na tumbuizi kwa masikio yenye kuisikia (Kihore, 1978).

Abdullazizi (1969) anaendelea kueleza kwamba, Mathias Mnyampala alipata kusifika sana katika tasnia ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili baada ya kuanzisha utanzu wa Ngojera na kuchapishwa katika *Ngonjera za UKUTA* namba moja na mbili. Aina hii ya mashairi ni ya majibizano baina ya watu wawili na kuendelea, jambo ambalo huipa sifa za sanaa za maonesho. Hata, hivyo katika maelezo yao Mulokozi na Sengo (1995) wanaeleza kwamba, Mnyampala hakuwa mwanzilishi wa utunzi wa ngonjera kwa kuwa zilikuwepo tangu katika kipindi cha usimulizi pale mwanadamu alipoanza tu kutumia lugha na kuwasiliana. Jambo jema alilolifanya Mnyampala ni kuuingiza utanzu wa Ngonjera katika maandishi ambayo tunayaona katika *Ngonjera za UKUTA* namba moja na mbili.

Maelezo yanayotolewa katika usuli huu yanaonesha kwamba, Mathias Mnyampala anatunga mashairi ambayo yanafanana na yale ya Shaaban Robert hasa katika kipengele cha fani ambapo tumeona naye pia akitumia utunzi wa mashairi ya kufuata kanuni za urari wa vina na mizani. Pengine inawezekana kukawa na ukaribu wa dhamira na maudhui katika utunzi wa kazi za wawili hawa. Hili ndilo jambo ambalo tulikusudia kulifanya katika kazi yetu hii kwa kulinganisha na kulinganua nafasi ya mwanamke inavyojitokeza na kusawiriwa katika kazi za washairi Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

Kwa upande wa mashairi ya Shaaban Robert ni Momanyi (2001) ndio aliyechambua nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert katika ngazi ya makala.

Makala yake yamekuwa ni dira na mwelekeo wetu katika kutaka kulinganisha na kulinganua nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na yale ya Mathias Mnyampala. Kuhusu mashairi ya Mathias Mnyampala hatujakutana na mtafiti au mhakiki ambaye amechunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi hayo jambo ambalo limetuvutia sana kuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kulizungumzia suala hili. Si watu wa mwanzo katika kulizungumzia suala hili tu bali pia watu wa mwanzo kwa kulinganisha na kulinganua mashairi ya nguli hawa wawili wa ushairi wa Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu umefanywa ili kulinganisha na kulinganua nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti na uhakiki kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii umefanywa kwa kiasi kikubwa katika kazi za Shaaban Robert za riwaya kuliko katika mashairi yake (Momanyi, 2001). Kwa upande wa mashairi ya Mathias Mnyampala hatujakutana na mtafiti hata mmoja ambaye amechambua au kuhakiki masuala ya kijinsia katika mashairi hayo. Baada ya kulifahamu hili, Momanyi (2001) aliamua kuandika makala juu ya nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert. Katika makala yake alionesha kwamba, Shaaban Robert anamsawiri mwanamke katika hali chanya na hali hasi. Kwa bahati mbaya sana alishindwa kueleza kwa undani ni kwa vipi mwanamke anasawiriwa katika hali hizo mbili na badala yake akaishia kugusiagusia tu.

Si hivyo tu, bali pia hakuna mtafiti yeyote ambaye amefanya utafiti wake kwa nia ya kulinganisha usawiri wa nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na

mashairi ya Mathias Mnyampala ili kupata uelewa mpana zaidi kuhusu nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili. Tunayasema haya kwa sababu, watunzi hawa wawili wanasifika na kuheshimika sana katika utunzi wa mashairi, kwa hivyo kutathimini usawiri wao wa nafasi ya mwanamke umetupatia uelewa mpana zaidi wa masuala ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, katika tasinifu hii tumechambua na kuhakiki kwa kina nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na kulinganisha na kulinganua na mashairi ya Mathias Mnyampala.

1.2 Malengo ya Utafiti

Utafifi huu utakamilika baada ya kukamilika kwa lengo kuu moja na madhumuni mahususi matatu. Lengo kuu na mdhumuni mahususi ni haya yafuatayo:

1.2.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kulinganisha nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ili kufahamu falsafa na mtazamo wa wasanii hawa juu ya nafasi ya mwanamke katika jamii.

1.2.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu una jumla ya malengo mahususi matatu ambayo ni:

1. Kulinganisha na kulinganua usawiri wa nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na yale ya Mathias Mnyampala.

2. Kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha ya kisanaa inayotumiwa na Shaaban Robert na Mathias Mnyampala katika kusawiri nafasi ya mwanamke.

3. Kubainisha falsafa ya Shaaban Robert na ile ya Mathias Mnyampala juu ya nafasi waliyompa mwanamke katika mashairi yao.

1.2.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unakusudia kujibu maswali yafuatayo:

1. Usawiri wa nafasi ya mwanamke unalingana na kutofautiana vipi katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala?
2. Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanafanana na kutofautiana vipi katika matumizi ya lugha ya kisanaa wanaposawiri nafasi ya mwanamke?
3. Ni ipi Falsafa ya Shaaban Robert na ile ya Mathias Mnyampala juu ya nafasi waliyompa mwanamke katika mashairi yao?

1.3 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kwa wanataalimu wote wanaojihusisha na masuala ya fasihi ya Kiswahili hususani Ushairi wa Kiswahili. Wanafunzi wa masuala ya fasihi watautumia utafiti huu katika kujifunza namna ushairi ulivyo na uwezo wa kusawiri nafasi ya mwanamke katika jamii.

Kwa watafiti wa masuala ya fasihi watauona utafiti huu kama sehemu muhimu ya wao kupata maeneo zaidi ya kufanyia utafiti katika kazi za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Shaaban Robert ameandika kazi nyingi mno ambazo zinahitaji kufanyiwa uhakiki na uchambuzi zaidi wa kitaaluma. Kupitia utafiti huu, watafiti wanaweza kuyaona maeneo mbalimbali ya kuyashughulikia kwa kuyafanyia utafiti.

Wahadhiri wa vyuo vikuu watautumia utafiti huu kama rejeleo muhimu katika kuandaa vitabu, makala, na insha kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wao. Hii itawafanya wasipate taabu ya kusoma kitabu chochote cha Shaaban Robert na kutoka patupu na badala yake, maelezo yaliyotolewa katika uchambuzi wetu ni darasa tosha

kwao. Watalaamu wa masuala ya jinsia pamoja na wanaharakati wa masuala hayo watauona utafiti huu kuwa ni sehemu ya kutoa elimu kwa umma wa wasomaji kuhusu masuala la kijinsia katika jamii.

Utafiti huu utakuwa na umuhimu wa kubainisha falsafa ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kuhusu nafasi ya Mwanamke katika jamii ya Watanzania. Yapo baadhi ya maandishi ambayo yameeleza kwa ufupi kuhusu mtazamo wa Shaaban Robert kwa wanawake (Senkoro, 1988). Hata hivyo, maandishi hayo yamegusia tu juu ya mtazamo wa mwandishi Shaaban Robert kuhusu wanawake bila ya kuyafanyia uchambuzi wa kina. Utafiti huu umechunguza kwa kina kuhusu falsafa ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kwa wanawake na nafasi yao katika jamii.

1.4 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi yaliyotungwa na Shaaban Robert na Mathias Mnyampala tu. Katika utafiti huu hatukuzungumzia riwaya pamoja na insha alizotunga Shaaban Robert bali tumeshughulikia diwani zake za *Pambo la Lugha* na *Ashiki Kitabu Hiki* peke yake. Kwa upande wa Mnyampala tumetumia kazi zake za *Waadhi wa Ushairi* na *Ngonjera za UKUTA namba Moja*. Pia, tathimini ya masuala ya kijinsia- nafasi ya mwanamke katika kazi hizo imefanywa kifasihi tu na si vinginevyo. Ni vema ikaeleweka kwamba, nafasi ya mwanamke katika jamii inaweza kuelezwa kwa namna nyingi kama vile kisiasa, Kitaaluma za Maendeleo, Kisosholojia na kadhalika. Sisi tumetathimini nafasi ya mwanamke katika kazi teule kwa mtazamo wa kifasihi.

1.5 Matatizo ya Utafiti na Utatuzi Wake

Utafiti huu unategemea kukumbana na matatizo kadhaa; kwanza ni suala la pesa, mazingara na ugeni wa mtafiti katika nchi ya Tanzania. Kwa sababu mtafiti anatokea Libya hivyo mazingira ya Tanzania yatakuwa magumu kwake na pia kuelewa mila na desturi za Watanzania kwa haraka na jinsi ya kukabiliana na hali hiyo ili kupata data zinazofaa kujibu maswali ya utafiti. Hata hivyo, changamoto hizi zilitatuliwa kwa mtafiti kutafuta mtafiti msaidizi ambaye alimuongoza katika mazingira haya mageni kwake. Mtafiti msaidizi alimsaidia katika zoezi la kukusanya data pamoja na kumfundisha baadhi ya mila na desturi za jamii ya Waswahili.

1.6 Hitimishi

Sura hii imewasilisha vipengele vinavyohusu utangulizi wa utafiti. Vipengele hivyo ni usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahususi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, matatizo na utatuzi wa matatizo ya utafiti. Sura inayofuata ni ya pili ambayo inawasilisha utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.

SURA YA PILI

UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetalii kazi tangulizi ambazo zimetafiti na kuhakiki nafasi ya mwanamke katika hususani zile za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Kwa hakika, kazi nyingi za uhakiki zimefanywa kuhusu maandishi ya Shaaban Robert. Miongoni mwa wachambuzi na wahakiki hao ni Kezilahabi (1976a), Kezilahabi (1983), Njogu na Chimerah (1999), Momanyi (2001), Twaib (2009) na Chuwachuwa (2011). Lakini katika tafiti zao hawakulenga kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert. Watafiti hao walikuwa na malengo tofauti na ya utafiti wetu lakini wamedokeza mambo ya msingi ambayo yatatusaidia katika utafiti wetu. Maelezo zaidi yanatolewa katika sehemu inayofuata.

2.1 Ushairi wa Shaaban Robert

Shaaban Robert alizaliwa tarehe 1 mwezi wa kwanza mwaka 1909. Shaaban Robert alianza shule mwaka 1922 na kumaliza 1926 katika shule ya Kichwele ambayo kwa sasa inafahamika kama Uhuru Mchanganyiko. Alipenda sana kusoma na kujiendeleza kielimu lakini jitihada zake hazikuzaa matunda kwa haraka kwa sababu ziliporwa na wakoloni kwa lengo la kumtumia kama chombo cha kutawalia. Hata hivyo mwaka 1932 aliendelea na masomo kwa njia ya posta ambapo mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya Fasihi. Mwaka 1936-37 alitunukiwa cheti cha *English Level*. Ni dhahiri kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye juhudi kubwa katika kujiendeleza kielimu na kama si wakoloni angalifika katika ngazi za juu zaidi.

Ilipofika mwaka 1926 alianza kazi katika idara ya Forodha Tanga. Hapo alidumu kwa miaka takribani 18. Mwaka 1944-1946 alihamishiwa Idara ya Wanyamapori huko Mpwapwa. Mwaka 1946 alirudishwa Tanga na kuwa Afisa Ardhi wa jimbo la Tanga. Aidha barua zake zinaonesha pia aliwahi kufanya kazi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam na Kisiju. Shaaban Robert alifariki tarehe 20.6.1964 na kuzikwa huko Vibambani tarehe 21.6.1962.

Senkoro (1968) anaeleza juu ya Mwamko wa kisiasa katika mashairi ya Shaaban Robert na kwamba, nguli huyu wa fasihi ya Kiswahili alikuwa ni mtaalamu wa kutumia lugha na mandhari ya kuhamasisha umma kudai haki zao bila ya mdaiwa kutambua hilo kwa haraka. Katika *Mashairi na Insha* kwa mfano, tunaona namna Shaaban Robert alivyo bingwa wa kuwasilisha dhamira za kisiasa katika mashairi yake kwa kutumia lugha ya kisiasa.

Mawazo haya ya Senkoro (1968) tunakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa kwa kuwa si yeye wa kwanza kumsifu Shaaban Robert kuwa ni mtunzi mashuhuri katika utumizi wa lugha ya Kiswahili katika kazi zake. Mawazo haya yanaungwa mkono na Njogu na Chimerah (1999), Wamitila (2008) na Ndulute (1987). Hata hivyo, halikuwa lengo la Senkoro (1968) kuhakiki nafasi ya mwanamke katika kazi za kishairi za Shaaban Robert lakini ametupatia mwanga wa kufahamu kwamba, Shaaban Robert ni bingwa wa matumizi ya lugha ya kisanaa katika utunzi wake wa mashairi. Nasi tumeyasoma mashairi yake kwa utulivu ili kuona namna anavyomsawiri mwanamke kupitia lugha hiyo ya kisanaa na kulinganisha na Mathias Mnyampala.

Maganga (1971) anaeleza kwamba, Shaaban Robert ni mtu ambaye alikuwa na mawazo ya kimapinduzi ambayo yalilenga kumkomboa kila mtanzania hususani mwanamke kutokana na mateso mbalimbali yanayomkumba katika jamii. Shaaban Robert anaonesha kwamba, mwanamke ndiye anayebeba ujauzito wa mtoto kwa miezi tisa na baadaye kumlea mtoto huyo mpaka akaweza kujitegemea yeye mwenyewe. Katika mazingira mengine mwanamke huachiwa majukumu ya kulea watoto peke yake huku mwanaume akiishia katika ulevi na anasa nyingine za kidunia. Shaaban Robert aliipinga hali hii na kuitaka jamii kumhurumia mama na kumpatia msaada wowote atakaouhitaji ili aishi maisha mazuri.

Mawazo ya Maganga (1971) hapo juu yanaonesha kwamba, Shaaban Robert amempatia mwanamke nafasi ya ulezi na huruma katika jamii huku mwanamme akionekana kutokuwa na sifa hizo. Mawazo haya tumeyachukua na kuyafanyia utafiti wa kina ili kuona ni kwa vipi mwanamke anatekeleza majukumu haya katika kazi za Shaaban Robert huku tukilinganisha na yale ya Mathias Mnyampala.

Ndulute (1994) aliandika juu ya ushairi wa Shaaban Robert na kujadili mambo mengi kuhusu mashairi hayo. Kwa mfano, alieleza juu ya fani na maudhui kwa ujumla wake kama inavyosawiriwa na Shaaban Robert. Katika maelezo yake amegusia kwamba, Shaaban Robert anazungumzia masuala ya jinsia katika jamii akionesha kwamba, mwanamke ni kiumbe ambaye anastahili kupatiwa heshima kubwa katika jamii kutokana na mambo mbalimbali anayoifanyia jamii katika maisha yake ya kila siku. Ingawa, Ndulute (ameshatajwa) hakuzamia katika kueleza ni kwa vipi sifa hizo anazopewa mwanamke zinajitokeza katika kazi hizo za Shaaban Robert lakini ametufungua macho kwamba, nafasi ya mwanamke inajadiliwa na

kujitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert. Tumefanya utafiti wa ndani zaidi ili kuonesha nafasi aliyopewa mwanamke katika mashairi hayo pamoja na kuyalinganisha na kulinganua na yale ya Mathias Mnyampala.

Sengo (1975) aliandika juu ya mada isemayo, *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi yake*. Katika uhakiki huu, Shaaban Robert anaelezwa kuwa ni mtu ambaye alijali sana ubinadamu katika jamii. Alipenda kuona kila mtu anapata heshima yake, haki zake na kutendeana mema kati ya wanadamu katika jamii. Mawazo haya yalikuja katika kipindi ambacho Tanganyika ilikuwa imetawaliwa na Wakoloni ambao hawakujali haki za Wanatanganyika. Kwa mantiki hiyo Shaaban Robert aliwataka Wakoloni hao kuwapatia wananchi haki zao pamoja na kuwaheshimu. Maelezo haya ya Sengo (1975) yana umuhimu mkubwa katika kuujenga utafiti wetu kwa sababu yanamwelezea Shaaban Robert kama mtetezi wa haki katika jamii. Kutokana na hili tunaona kwamba, Shaaban Robert alitetea haki za watu wote katika jamii wakiwamo wanawake na wanaume.

Kwa msingi huo basi, katika utafiti wetu tumechunguza nafasi aliyopewa mwanamke katika kudai na kupatiwa haki zake za msingi katika jamii iliyokuwa ikitawaliwa na Wakoloni. Ingawa uhakiki wa Sengo (ameshatajwa) haukulenga kuchunguza nafasi aliyopewa mwanamke katika maandishi ya Shaaban Robert lakini umetupatia ufahamu wa kutosha, kwamba nafasi ya mwanamke inatokeza na kujadiliwa katika ushairi wa Shaaban Robert. Katika utafiti wetu tumechunguza kwa kina ni kwa vipi nafasi ya mwanamke inajitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

Kezilahabi (1976a) aliandika kazi yake ambayo aliipa jina la *Ushairi wa Shaaban Robert*. Katika kazi hii Kezilahabi ameanza kwa kumsifu Shaaban Robert kuwa ni mtunzi mashuhuri na adhwimu katika tasinia ya fasihi ya Kiswahili asiyekuwa na mfano katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Jambo kubwa lililomvutia Kezilahabi mpaka kuamua kumsifu Shaaban Robert ni ule ubingwa wake wa matumizi ya lugha ya kisanaa ambao pia umeelezwa na Senkoro (1968). Anasema kwamba, Shaaban Robert alikuwa ni bingwa wa uteuzi wa misamiati ambao watunzi wa baada yake hawawezi kabisa kujinasibisha naye hata kidogo.

Hata hivyo, Kezilahabi (1976a) anaeleza kwamba, Shaaban Robert alijikita katika kueleza baadhi ya mambo ambayo katika ulimwengu wa kawaida hayawezekani kutokea. Miongoni mwa mwambo hayo ni lile na kutolea mifano ya watu wema wasio na makosa hata kidogo na watu waovu tu wasio na wema hata kidogo. Hili ni jambo ambalo halina uhalisia katika jamii. Suala hili tunakubaliana nalo na tunaona kwamba, linatoa mchango muhimu wa kukamilisha utafiti wetu. Hata hivyo, Kezilahabi hakuelewa kwamba, utunzi wa Shaaban Robert ulikuwa hivyo kwa nia ya kuhimiza mema na kukataza maovu katika jamii. Haina maana kwamba, Shaaban Robert alikuwa hatambui kwamba, hakuna mtu mwema tu asiye na chembe ya uovu na hakuna pia mtu muovu tu asiye na chembe ya wema ila alifanya hivyo kwa makusudi maalumu. Mawazo haya tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu ili kuona ni kwa namna gani yanamlenga mwanamke na kulinganisha na kulinganua na mashairi ya Mathias Mnyampala.

Kezilahabi (1976b) aliandika tasinifu yake ya Uzamili juu ya Shaaban “Robert Mwandishi wa Riwaya.” Ingawa kazi hii ilihusu riwaya lakini pia alitumia kazi moja

ya kishairi iitwayo *Mapenzi Bora* sambamba na riwaya za Shaaban Robert. Pamoja na mambo mengi ambayo ameyaonesha katika tasinifu yake, amekiri kwamba, mama ni kiumbe ambaye amesawiriwa na Shaaban Robert kama kiumbe mvumilivu na mwenye unyenyekevu mkubwa katika maisha. Kutokana na hali hii, mwanamke amekuwa kiigizo chema cha ukarimu, upole na hekima katika jamii na kuufanya ulimwengu kuwa mahali salama pa kuishi watu wote. Lau ingelitokezea mwanamke kukosa sifa hizo basi dunia ingekuwa mahali pabaya pa kuishi. Mawazo haya tunayakubali na tumeyafanyia kazi katika utafiti wetu ili kueleza kwa kina namna mwanamke anavyosawiriwa katika mashairi ya Shaaban Robert na yale ya Mathias Mnyampala.

Momanyi (2001) aliyandika makala juu ya nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Katika makala yake hii alionesha kuwa Shaaban Robert anamsawiri mwanamke katika hali mbili. Hali ya kwanza ni ile inayomtazama mwanamke kama kiumbe ambaye ni mlezi katika jamii, mkarimu, mpole, mnyenyekevu, mwenye huruma na kadhalika. Hali ya pili ni ile ambayo inamtazama mwanamke kama kiumbe duni katika jamii. Mawazo haya ni muafaka kwa sababu yanaeleza mambo kama yanavyotokea katika jamii. Wapo wanawake ambao wanafanya mambo yanayokubalika katika jamii na wapo wengine ambao wanafanya yale yasiyokubalika katika jamii. Huu ndio uhalisia katika maisha ya jamii na msanii makini ni lazima ayasawiri hivyo. Mawazo ya Momanyi ni msingi muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu na tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti huu.

Hata hivyo, makala yake ilikuwa finyu mno kiasi cha kushindwa kuieleza kinaganaga nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Utafiti huu

tulioufanya umelenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anaitumia sanaa yake kuwasilisha falsafa na mtazamo wake kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii huku tukimlinganisha na kumlinganua na Mathias Mnyampala.

2.2 Ushairi wa Mathias Mnyampala

Mathias Mnyampala alizaliwa mwaka wa 1917 na kufariki dunia mwaka wa 1969. Alizaliwa katika kitongoji cha Muntundya katika kijiji cha Ihumwa katika wilaya ya Chamwino katika mkoa wa Dodoma. Alifanya kazi kama karani wa kodi katika serikali ya kikoloni na na baada ya uhuru aliendelea na kazi ya utumishi wa umma katika mahakama kama hakimu. Aliandika vitabu zaidi ya 25. Alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa UKUTA katika mwaka wa 1961(Abdulazizi, 1969). Kazi zake za ushairi hasa utunzi wa Ngonjera ulimfanya kupata sifa nyingi sana katika tasinia ya fasihi ya Kiswahili. Wapo watafiti kadhaa ambao wametafiti na kuhakiki kazi zake ingawa si kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa Shaaban Robert. Kati ya waliohakiki na kutafiti kazi zake ni:

Abdullazizi (1969) ambaye aliandika juu ya ukumbusho wa Marehemu Sheikh Mathias E. Mnyampala. Katika makala yake haya, anamsifu Mnyampala kuwa ni mtunzi mashuhuri ambaye alianzisha utanzu wa ngonjera katika ushairi wa Kiswahili na kueleza dhamira mbalimbali. Miongoni mwa dhamira hizo ni zile zinazohusu umoja na mshikamano katika jamii, umuhimu wa kuishi Kijamaa na Kujitegemea, malezi na maadili mema katika jamii, uongozi bora na imara, haki na usawa katika jamii na kadhalika. Mawazo ya Abdulazizi (1969) ni muhimu katika kuupeleka mbele utafiti huu kwa sababu unagusia mambo ambayo ni muhimu kwetu

kuyachunguza kwa kina. Anapotaja masuala ya umoja na mshikamano katika jamii bila shaka anazungumzia umoja baina ya mwanamke na mwanamme. Tumefanya utafiti wa kina katika mashairi ya Mnyampala ili kuona nafasi anayompa mwanamke katika kazi zake na kulinganisha na kulinganua na zile za Shaaban Robert.

Kihore (1978) aliandika makala yake juu ya *Waadhi wa Ushairi* diwani ya mashairi ya Mathias Mnyampala. Katika uchambuzi wake amebainisha vipengele mbalimbali vya kifani na kimaudhui. Kwa upande wa fani, anaonesha kwamba, Mathias Mnyampala ni bingwa wa kuandika mashairi ambayo yanafuata urari wa vina na mizani (Mulokozi na Kahigi, 1979). Kwa upande wa maudhui, anaeleza kwamba, Mathias Mnyampala anaeleza juu ya dhaimira za ujenzi wa jamii mpya iliyo na uongozi bora, usawa, haki, heshima kwa watu wake, upendo, amani na kuhurumiana baina ya wanadamu. Ingawa Kihore (1978) hakuwa na lengo la kuzungumzia nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Mathias Mnyampala lakini yapo mambo kadhaa ambayo ameyagusia na yanatuelekeza kufahamu kwamba, katika mashairi ya Mnyampala kuna usawiri wa nafasi ya mwanamke katika jamii. Tumechunguza kwa kina na kuonesha ni kwa vipi nafasi ya mwanamke inajitokeza katika mashairi ya Mathias Mnyampala na kulinganisha na kulinganua na mashairi ya Shaaban Robert.

Ndulute (1985) anaeleza kwamba, Mathias Mnyampala ni miongoni mwa washairi wa Kiswahili ambaye ameacha utajiri mkubwa sana katika tasinia ya ushairi wa Kiswahili. Kwanza alianzisha utanzu wa Ngonjera ambao unaonesha kwamba, ushairi ni tukio halisi ambalo linaweza kutendwa kwa kuigizwa kama ilivyo katika utanzu wa tamthilia na maigizo. Pili alikuwa ni miongoni mwa washairi ambao amedumisha kanuni za utunzi wa ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia umbo lake la

asili. Mawazo haya tunakubaliana nayo na kwamba, yanatoa mchango muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu.

Hata hivyo, si kweli kwamba, Mnyampala ndiye aliyeaanzisha utanzu wa ngonjera kwa kuwa utanzu huu ulikuwepo tangu siku nyingi za kipindi cha usimulizi ila ingefaa kusema kwamba, yeye ameutia katika maandishi. Nia kuu ya utafiti huu ni kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kwa hivyo mawazo ya Ndulute (ametajwa) hapo juu yametupatia muongozo kamili wa kufanikisha nia yetu hii.

2.3 Mkabala wa Kinadharia

Katika sehemu hii tunaeleza nadharia ambayo imetumika katika kuwezesha kukamilika kwa madhumuni mahusui ya utafiti wetu. Nadharia hiyo ni ile ya Ufeministi ambayo inafafanuliwa kwa kina hapa chini.

2.3.1 Nadharia ya Ufeministi

Kuna nadharia nyingi ambazo hutumika kuchambua na kuhakiki kazi za kifasihi. Nadharia hizo hutumiwa ili kutoa muongozo kamili juu ya namna kazi za mwandishi fulani zitakavyochambuliwa na kuhakikiwa. Kwa mfano, katika utafiti wetu tulikusudia kutafiti nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kwa hivyo ni lazima tutumie nadharia ambayo inaelezea na kufafanua masuala ya jinsia yalivyo, yanavyotokea na yanavyotakiwa kuwa katika jamii. Hivyo basi, katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike (Feminist Psychoanalytic Theory). Hii ni nadharia iliyoibuka kutokana na kazi zilizoasisiwa na Jacques Lacan kama alivyonukuliwwa

na Momanyi (2001). Nadharia hii inahakiki matini katika misingi ya uchanganuzi nafsia. Huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume.

Katika utaratibu fiche, maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke hughubikwa na badala yake maumbo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusianao wowote na uhalisia wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususan kupitia lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, nafasi ya mwanamke imefungamana na lugha inayomzungumzia na lugha inayoashiria uana wake. Nafasi hii hufinyangwa na jamii kupitia asasi mbalimbali ili aweze kukubalika katika utaratibu huo wa kishara. Uchanganuzi nafsia katika mtazamo wa kike ni nadharia bia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya uana.

Sababu ya kuteua nadharia hii, ni kwamba wapo watafiti ambao pia wametumia nadharia hii katika kuchambua mahusiano ya mwanamke na mwanamume katika kazi za fasihi mfano Momanyi (2001). Hatimaye nadharia hii ilimweza kumfikisha kwenye mafanikio katika kuibua suala la ujinsia katika fasihi na kutimiza malengo yake ya utafiti. Aidha uhakiki wa kazi za fasihi kwa kutumia nadharia hii una wajibu wa kuzingatia kuwepo kwa taasubi za kiume zilizoimarishwa ndani ya utaratibu wa kiishara katika mfumo wa kuumeni. Taasubi hizo ndizo zinazomdunisha mwanamke na kumweka katika kitengo maalumu kijamii (Momanyi, 2001).

Maudhui ya nadharia hii yanaonesha kwamba, mwanamke ni kiumbe ambaye amedunishwa sana katika jamii kutokana na kushamiri kwa mfumo dume katika jamii. Mfumo dume katika jamii unamfanya mwanamke kuwa ni kiumbe aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumtumikia na kumstarehesha mwanaume kwa njia na namna mbalimbali (Momanyi, 2007). Kwa mfano, mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe wa kukaa nyumbani akifanya kazi za kupika chakula, kufua nguo, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, kulea watoto, kulea ndugu wa mume na kadhalika. Wakati mwanamke anatazamwa kwa namna hii, mwanaume ni kiumbe aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kufanya kazi za kuingiza kipato. Hali hii kwa hakika imemfanya mwanamke kuonekana kama kiumbe dhaifu mbele ya mwanamme kwa sababu mwanamke anafanya kazi ambazo haziingizi kipato na anategemea kipato cha mwanamme katika kuendeshea maisha yake. Hii ina maana kwamba, pasipokuwepo mwanaume basi mwanamke hawezi kuishi maisha mazuri.

Hivyo basi, tumeyatumia maudhui ya nadharia hii katika kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Nadharia hii imetusaidia kuona ni kwa vipi Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanaieleza nafasi ya mwanamke katika mashairi yao huku tukirejelea maudhui ya nadharia hii tuliyoiteua kuitumia.

2.4 Hitimishi

Utalii wa kazi tangulizi uliofanywa katika sura hii unaonesha kuwa, hakuna mtafiti aliyefanya utafiti wa kulinganisha na kulinganua nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Hili lilibainika baada ya sura

hii kutalii kazi tangulizi zilizotafiti ushairi wa Shaaban Robert na ushairi wa Mathias Mnyampala. Nadharia ya Ufeministi ndiyo iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu.

SURA YA TATU

NJIA ZA UTAFITI

3.0 Eneo la Utafiti

Babbie (1992) anaeleza kwamba, eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyikia au unakusudiwa kufanyikia. Katika eneo la utafiti ndipo data za utafiti hupatikana kwa mtafiti kufanya usaili, mahojiano, kushuhudia au kushiriki shughuli au tukio fulani pamoja na watafitiwa. Eneo la utafiti ni jiji la Dar es salaam na jiji la Tanga. Jiji la Dar es Salaam limeteuliwa kwa sababu ni mahali ambapo kunapatikana machapisho mbalimbali yanamuhusu Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kuliko sehemu nyingine yoyote ile katika Tanzania. Hii inatokana na ukweli kwamba, maktaba kubwa ambazo ndizo zenye machapisho yanayomuhusu Shaaban Robert yanapatikana. Nalo jiji la Tanga limeteuliwa kwa sababu ndipo Nyumbani kwa Shaaban Robert ambapo wanapatikana ndugu jamaa na marafiki ambao tumewasaili. Sehemu maalumu itakapofanyikia utafiti huu ni Vibambani nje kidogo ya jiji la Tanga. Pia tutafanya utafiti katika Manispaa ya Dodoma ambako ndiko nyumbani kwa Mathias Mnyampala na familia yake inapatikana huko. Maeneo haya matatu yametupatia data tunazozihitaji ili tuweze kufanikisha malengo ya utafiti wetu.

3.1 Kundi Lengwa

Kulingana na Cresswell (2009) kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kwa hiyo katika utafiti huu walengwa ni diwani mbili za Shaaban Robert ambazo ni *Pambo la Lugha* na *Ashiki Kitabu Hiki* na *Ngonjera za UKUTA* na *Waadhi wa Ushairi*. Katika kazi hizo mbili za kila mmoja ndimo tulikopata data za kueleza

namna Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanavyoisawiri nafasi ya mwanamke katika jamii. Kundi la pili litakuwa ni watoto, ndugu, jamaa na marafiki wa Shaaban Robert ambao wanapatika katika jiji la Tanga na wale wa Mathias Mnyampala wa Dodoma. Kundi la tatu ni wale ambao wametafiti kazi za wasanii hawa wawili katika utunzi wao wa mashairi.

Katika kundi hili la pili tutapata data zinazoeleza namna Shaaban Robert alivyokuwa akiishi na wanajamii wenzake katika familia yake na nje ya familia hususani mtazamo na matendo yake dhidi ya wanawake. Kundi la tatu litawahusu watafiti na wahakiki ambao wameshughulikia kazi za Shaaban Robert kwa namna moja au nyingine. Watafitiwa hawa walitueleza wao wanaionaje nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na yale ya Mathias Mnyampala walipokuwa wakiyasoma mashairi hayo katika harakati za kukamilisha malengo ya utafiti wao.

3.2 Sampuli ya Utafiti

Uteuzi wa sampuli ya utafiti kama unavyoelezwa na Young (1984) ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilisho cha kundi lote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima la watafitiwa. Sampuli ya utafiti huu imeganyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza linajumuisha diwani mbili za mashairi ya Shaaban Robert ambao ni *Pambo la Lugha* na *Ashiki Kitabu Hiki* na *Ngonjera za UKUTA* pamoja na *Waadhi wa Ushairi*. Kundi la pili ni la watafitiwa ambao ni watoto, ndugu, jamaa na marafiki wa Shaaban Robert ambao jumla yao ilikuwa ni 10 na kundi la tatu ni la watafitiwa ambao wameshughulikia kazi za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ambao jumla yao ni 10.

3.3 Mbinu za Kukusanyia Data

Katika kukusanya data za utafiti huu tumetumia mbinu tatu ambazo ni; mbinu ya usaili, hojaji na maktaba.

3.3.1 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data kwa mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa. Mtafiti huandaa maswali na kuyaandika katika dodoso kwa ajili ya kuwauliza watafitiwa wake ili kupata data zinaweza kusaidia kujibu maswali yake ya utafiti (Kothari, 2009). Tumeitumia mbinu hii kufanya usaili na watafitiwa ambao walishatafiti maandishi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kwa namna moja au nyingine. Watafitiwa hawa wametueleza ni kwa vipi Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanazungumzia nafasi ya mwanamke katika jamii. Mbinu hii ya usaili ni madhubuti katika kumpatia mtafiti data za kutosha kumwezesha kujibu maswali ya utafiti wake kwa muda mfupi (Borg na Gall, 2003). Vilevile, mbinu hii humsaidia mtafiti kupata data ambazo hapo awali alikuwa hajategemea kuzipata. Si hivyo tu bali pia, mbinu hii inamwezesha mtafiti kuuliza maswali ya ziada kutegemeana na msailiwa anavyojibu maswali yake. Hata hivyo, mapungufu ya mbinu hii ni kwamba, inatumia muda mrefu sana na mtafiti hawezi kupata data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi. Mapungufu ya mbinu hii yalitatuliwa na matumizi ya mbinu ya Hojaji.

3.3.2 Hojaji

Hojaji ni mbinu ya kukusanya data maskanini kwa mtafiti kuandaa maswali katika karatasi na kuacha wazi nafasi za kujazwa na watafitiwa pale watakapopatiwa hojaji hizo (Cohen na Wenzake, 2000). Mbinu hii humwezesha mtafiti kukusanya data

nyingi kwa muda mfupi kutoka kwa watafitiwa wengi tofauti na ilivyokuwa katika mbinu ya usaili. Pia, mbinu ya hojaji humwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwani wakati wahojiwa wanapokuwa wanajaza hojaji yeye huendelea na shughuli nyingine katika harakati za kukamilisha utafiti wake. Mapungufu ya mbinu hii ni kwamba, haifai kutumika kuwahoji watafitiwa ambao hawajui kusoma na kuandika. Upungufu huu unalituliwa na mbinu ya usaili ambayo tumeieleza hapo juu. Mbinu hii ilitumika kukusanya data kutoka kwa baadhi ya wataalamu wa fasihi ambao wametafiti kazi za ushairi za watunzi hawa wawili.

3.3.3 Mbinu ya Usomaji Makini

Hii ni mbinu ya utafiti inayomtaka mtafiti kusoma kazi alizoziteua kwa makini ili aweze kupata data anazokusudia zijibu maswali yake ya utafiti (Cresswell, 2009; Robson, 2007; Best na Khan, 1993). Kwa mantiki hii, mtafiti alisoma kazi nne za ushairi alizoziteua na kila alipokutana na aya, sentensi, au neno ambalo linahusiana na malengo ya utafiti alilinukuu katika daftari maalumu. Vilevile, mbinu hii ilitumika katika kukusanya data za upili kutoka katika machapisho mbalimbali yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzani, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

3.4 Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data hufanywa ili kuweza kukamilisha malengo ya utafiti na kuyawasilisha matokeo ya utafiti huo katika tasinifu (Inyani, 2002). Katika kuchambua data za utafiti huu tulitumia mbinu ya mkabala wa kidhamira. Mkabala huu unatoa maelekezo kwamba, katika kuchambua data za utafiti ni lazima hatua kuu nne zifuatwe (John, 2007). Hatua ya kwanza ni kukusanya data za utafiti kwa mujibu

wa kanuni mbalimbali zinazoongoza ukusanyaji wa data katika utafiti. Hatua ya pili ni kuzipanga data zilizokusanywa katika makundi kwa kadiri zinavyofanana na kuwiana. Hatua ya tatu ni kuhusianisha data za utafiti na madhumuni ya utafiti ili kuweza kuandaa mada kuu na ndogondogo ambazo husaidia kulifanya zoezi la uchambuzi wa data kuwa rahisi. Hatua ya mwisho ni kuchambua data za utafiti kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti husika.

Uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia hatua zote nne. Katika hatua ya kwanza tulizingatia kanuni zote za ukusanyaji wa data. Hii ndiyo hatua ya kwanza katika ukusanyaji wa data za utafiti. Huwezi kuchambua data kama hujakusanya, ndio maana hii ikawa ni hatua ya kwanza. Kanuni za ukusanyaji wa data ni zile zote zilizoelezwa katika sura hii ya tatu. Hatua ya pili ilikuwa ni kupanga data kulingana na vile zinavyohusiana na kufanana. Data zilizohusu nafasi ya mwanamke katika mashairi teule ziliwekwa katika kundi moja kutoka kwa kila mwandishi. Data zilizohusu matumizi ya lugha ya kisanaa katika kazi hizo za ushairi nazo ziliwekwa katika kundi moja. Na kundi la mwisho ni lile lililohusu data za falsafa za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala juu ya nafasi ya mwanamke. Hivyo basi katika kuchambua data za utafiti huu hatua zote nne tulizozieleza zitazingatiwa.

Katika hatua ya tatu tuliazipanga data za waandishi wote wawili kwa kuzichanganya zile zinazoeleza jambo moja na kisha kuunda mada kuu na mada ndogondogo zilizotuwezesha kufanya uchambuzi. Mada zilizotengenezwa katika sura ya nne zilizingatia madhumuni mahususi ya utafiti. Hatua ya mwisho ilikuwa ni kufanya uchambuzi na kujadili data za utafiti na kuunda sura ya nne ya tasinifu hii.

3.5 Kuaminika kwa Data za Utafiti

Mtafiti ametumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data za utafiti wake. Mapungufu ya mbinu moja ya kukusanyia data yalitatuliwa kwa haraka na mbinu nyingine na hivyo kuzifanya data zake kuaminika kwa wasomaji wake (Babbie, 1992). Mbinu ambazo tulizitumia katika kukusanya data ni mbinu za usaili, hojaji na usomaji makini. Vilevile, mkabala wa kidhamira ndio ambao umetumika katika kuchambua data za utafiti huu ambao bila shaka ni mkabala maarufu katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Hivyo, data za utafiti huu zinaaminiwa na wasomaji na watafiti wengine kwa sababu umefanywa kisayansi na kitaaluma.

3.6 Usahihi wa Data za Utafiti

Usahihi wa data za utafiti unatokana na kufuatwa kwa taratibu zote za utafiti husika kama ilivyoainishwa katika pendekezo la utafiti (Cohen na Wenzake, 2000). Mtafiti alihakikisha kwamba, mbinu za utafiti zilizoelezwa katika pendekezo la utafiti zinafuatwa na kuzingatiwa kwa makini tangu mwanzo wa utafiti huu mpaka mwisho. Mbinu hizi zilijadiliwa na kuimarishwa katika semina za uzamili na wataalamu wabobezi katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili kwa nia ya kuzifanya kuwa sahihi na imara zaidi.

3.7 Hitimisho

Mbinu za utafiti ndizo husaidia kupatikana kwa data zinazopelekea kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti na hatimaye lengo kuu. Sura hii imewasilisha vipengele vya eneo la utafiti, kikundi lengwa, sampuli ya utafiti na usampulishaji. Vipengele vingine ni mbinu za kukusanya data za usaili, hojaji na usomaji makini,

mbinu ya mkabala wa kinadharia ya uchambuzi wa data, kuaminika kwa mbinu za utafiti na usahihi wa data za utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.0 Utangulizi

Hii ni sura mama katika utafiti wetu kutokana na umuhimu wake. Sura hii ndiyo inayowasilisha mambo muhimu ambayo yanawezesha kutimizwa kwa malengo ya utafiti. Young (1984) anaeleza kuwa, utafiti hauwezi kukamilika mpaka pale matokeo ya utafiti huo yatakapowasilishwa kwa namna inayokubalika kitaaluma. Hivyo, uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu umefanywa kwa kurejelea madhumuni mahususi ambayo jumla yake ni matatu. Madhumuni mahususi ya kwanza yalilenga katika kulinganisha na kulinganua usawiri wa nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Madhumuni mahususi ya pili yalihusu kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha yanayotumiwa kumsawiri mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Madhumuni mahususi ya tatu na mwisho yalihusu kulinganisha na kulinganua falsafa ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala katika kumsawiri mwanamke. Baada ya utangulizi huu sasa tutazame madhumuni mahususi ya kwanza yalivyotimizwa katika utafiti huu.

4.1 Usawiri wa Mwanamke katika Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala

Usawiri wa mwanamke katika kazi za fasihi umefanywa na wahakiki pamoja na watunzi mbalimbali wa kazi za fasihi za ushairi, riwaya, tamthilia, nyimbo, ngano na michezo ya kuchekesha (Momanyi, 2001). Usawiri wa mwanamke katika kazi hizo hujitokeza kwa namna anuai ambazo ni faafu au chanya na zisizofaafu au hasi.

Mathalani, mwanamke husawiriwa kama chombo cha kumstarehesha mwanaume, kiumbe asiyekuwa mwaminifu, msaliti, Malaya na kiumbe tegemezi kwa mwanaume. Pia mwanamke husawiriwa kama kiumbe mchapakazi, mwadilifu, mama na mlezi wa familia, mzalishaji mali, na kiongozi wa familia (Ramadhani, 2013).

4.1.1 Mwanamke kama Chombo cha Starehe

Mwanamke kusawiriwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume ni dhamira kuu katika kazi nyingi za fasihi hasa kutokana na mfumo dume uliopo katika maisha (Moore, 1998). Mfumo dume ni ile hali ya wanaume kuonekana kuwa ndio watu wa tabaka la juu katika jamii na wanapaswa kupatiwa matunzo na heshima ya hali ya juu kutoka kwa wanawake. Khatibu (1985) anatoa mfano wa *Utenzi wa Mwanakupona* kama kielezeo sahihi cha maisha ya mwanamke mbele ya mumewe tangu anapoolewa mpaka kufarikiana. Anasema, mwanamke anatakiwa ampokee mumewe anapotoka kazini, amkaribishe ndani na kumketisha kitako, amkandekande na kumchua ili kupunguza maumivu, amwandalie maji ya kukoga na kumkogesha na kisha ampake mafuta na kumchana nywele miongoni mwa mengi ya hayo. Mathias Mnyampala anamsawiri mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume katika shairi la “Tamaa.” Anasema:

> Na awe mzee sana, meno kinywani hanayo
> Hawezi kitu tafuna, sababu ni kibogoyo
> Lakini nyama kiona, humpaparika moyo
> Tamaa ni wayo wayo, haina moyo kuchoka
>
> Akiona msichana, moyo una wayo wayo
> Pale wanapokutana, maneno huwa ya payo
> Vipi wewe nguvu huna, ukatamanisha moyo
> Tamaa ni wayo wayo, haina moyo kuchoka (Uk. 18).

Katika beti hizo mbili za shairi, kunaoneshwa kuwa mwanamke ni chombo cha starehe kwa mwanaume hasa starehe za Kingono. Mtu mzima ambaye ameshazeeka na kutokuwa na nguvu bado anaonekana kumtaka mwanamke na kustarehe naye kingono. Kwa hakika, mwanaume huyo hawezi kufanya tendo hilo kwa ufanisi unaotegemewa kwa sababu ya kukosa nguvu za kufanya hivyo. Swali tunalojiuliza ni kuwa, kwa nini mwanaume huyo amtake mwanamke ambaye ni msichana mdogo ambaye damu yake bado inachemka? Jibu la swali hili si jingine bali ni kuwa mwanaume huyu anamuona mwanamke kama chombo cha starehe tena starehe kwa mwanaume. Ni starehe kwa mwanaume kwa sababu, Mzee kama huyo hawezi kumstarehesha mwanamke kutokana na kukosa nguvu za kufanya hivyo. Hivyo, katika hali kama hii starehe inakuwa si ya watu wawili bali mtu mmoja tu. Mkazi mmoja wa "Area C" katika Manispaa ya Dodoma alitueleza kuwa, katika jamii ya Wagogo mwanaume ni mtu asiyetarajiwa kuzeeka katika masuala ya mapenzi na ngono kama ilivyo kwa mwanamke. Mwanaume atastaafu kazi lakini si ngono. Ndio maana karibu kila mzee wa Kigogo anakuwa na mahusiano ya kingono na binti asiye wa makamo yake.

Mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume inabainika pia katika mashairi ya Shaaban Robert. Anamchora mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume kutokana na maumbile yake. Mwili wa mwanamke umeumbwa kwa namna ambayo inamwezesha mwanaume kustarehe vizuri bila wasiwasi wowote. Katika shairi la "Urafiki" lililopo ndani ya *Pambo la Lugha* anasema:

> Umbo la Kupendeza, kama la malaika,
> Sura ya kufurahisha, kama ile ya pepo,
> Umbo la takaso, kama mbingu na mwezi,
> Hulingani na mkadi, labda lulu bahari (Uk. 32).

Ubeti huu unamaanisha kuwa mwanamke ni chombo cha starehe kwa mwanaume kutokana na kuwa na umbo zuri la kumburudisha na kumstarehesha mwanaume. Mathalani, pale mshairi anaposema kuwa mwanamke ana umbo la kupendeza kama la malaika, tunapata hisia kuwa umbo hilo ni la kumpendezesha na kumfurahisha mwanaume. Hata msitari wa pili nao unaeleza jambo hilo hilo. Mwanamke anasawiriwa kama chombo ambacho mwanaume akikitazama tu basi anapata starehe ya ajabu. Hata katika jamii ya leo kila mwanaume hupenda kuoa mwanamke ambaye ana umbo na sura ya kuvutia watu pale wamtazamapo. Mwanamke huyo anapopita barabarani na kila mtu hasa wanaume kuanza kumshangaa basi mume au rafiki wa mwanamke huyo hupata raha ya ajabu kabisa. Usaili tuliofanya na mkazi mmoja wa eneo la Kange katika jiji la Tanga kuhusiana na mwanamke kuwa chombo cha starehe kwa wanaume alikiri kuwa ni kitu cha kweli na kinatokea katika jamii. Aalieleza kuwa katika Jiji la Tanga hivi sasa wapo wanawake ambao wanafanya kazi ya kuuza miili yao na wakionekana katika barabara kadhaa usiku wakiwa nusu uchi. Nusu uchi hiyo huwafanya wanaume kuwatamani na kwenda kustarehe nao.

Hali hii ndiyo inayotufanya tuamini kuwa mwanamke anatazamwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume. Imefika mahali katika jamii kuona baadhi ya wanaume wakiwazuia wanawake zao kufanya kazi ngumu na kuwataka kukaa nyumbani wakisaidiwa kazi na wafanyakazi wa ndani. Lengo hasa la kufanya hivyo, ni kumvundika mwanamke ili aive vizuri na kuvutia kila siku. Katika usaili tulioufanya na Mzee Sengo alieleza kuwa, mwanamke anapokuwa ameiva na kupendeza vizuri humfanya mwanaume kuvutiwa kufanya ngono na mwanamke huyo. Msailiwa mmoja katika barabara ya Kumi na Nne jijini Tanga alifafanua kuwa mwanamke

kuvundikwa aive ndio sahihi yake. Hata kule kutakiwa mwanamke kujigubika nguo mwili mzima ni kuvifanya viungo vyake vipate jua na kupauka. Kila mara vinapofunikwa ndivyo maungo ya mwanamke huiva na kupendeza. Hii inaonesha kuwa ikiwa mwanamke hafuniki maungo yake hupauka na kutomvutia mwanaume kingono. Kwa mantiki yote hiyo, inaonesha kuwa mwanamke ni chombo cha starehe kwa mwanaume. Ramadhani (2013) anasema kuwa, nyimbo za Taarab ya Mipasho za Mzee Yusuf Mzee kwa mfano, zinamchora mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume katika maisha yake yote.

Mjadala uliofanyika hapo juu unaonesha kuwa, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanafanana katika kumsawiri mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume. Tafauti yao ni kuwa Mathias Mnyampala ameonesha bayana kuwa mwanaume ni mtu anayemchukulia mwanamke kama chombo cha starehe hasa za ngono. Hili limeonekana pale mzee mwanaume asiyekuwa na nguvu kuonekana akiwa bado anatamani kuwa na mahusiano na msichana mdogo. Shaaban Robert kwa upande wake amemsawiri mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume kutokana na umbo na sura aliyonayo mwanamke. Hata hivyo, kwa pamoja watunzi wote hawa wawili wanamsawiri mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume.

4.1.2 Mwanamke ni Mpole, Mnyenyekevu kwa Mwanaume

Mwanamke ni kiumbe ambaye anatarajiwa kuwa ni mtu mpole na mnyenyekevu kwa mwanaume katika maisha ya kila siku. Upole na unyenyekevu huo utaonekana katika lugha anayotumia pale anapoongea na mwanaume. Mwanamke hategemewi

kubishana au kutoa lugha ya matusi kwa mumewe au mwanaume mwingine yoyote katika jamii. Shaaban Robert anasema:

> Mke akiwa mbishi, wa kushindana kusema
> Na majivuno na mashi, na ulimi wake pima
> Hata kama wala pishi, wali na kilo ya nyama
> Utajiona aishi, duniani huna kima (uk. 22).

Mwanamke anapokuwa ni mbishi na tena mwenye majivuno huyafanya maisha ya mwanaume kuwa magumu sana. Momanyi (2001) anaeleza kuwa ni jambo la ajabu kuona mwanamke akitakiwa kutokuwa mbishi na mwenye majivuno na mwanaume asionywe juu ya mambo hayo. Anaona kuwa sifa hizo si nzuri kwa wanajamii wote na si kwa mwanamke pekee. Hata hivyo, ni mwanamke pekee anayetakwa kutokuwa na tabia hizo ili awe mnyenyekevu kwa mwanaume. Mtunzi anaonesha kuwa kama mwanamke atakuwa na tabia ya ubishi, majivuno na mwingi wa kusema sana basi mumewe atakosa raha ya kuishi duniani. Ikatokea mwanaume huyo kuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa wa kuweza kula kila anachotaka basi hawezi kunawiri kutokana na majivuno, ubishi na maneno ya mke wake. Katika hojaji moja kuliandikwa kwamba mwanaume yoyote anayetaka kuishi katika ndoa yake kwa amani ni vema akahakikisha kuwa anapata mke ambaye si mbishani na mwenye kusema sana.

Maelezo ya Shaaban Robert katika ubeti uliopo hapo juu yanaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye anaweza kuyafanya maisha ya mwanaume kuwa mazuri au mabaya. Hili tunalipata pale anaposema kuwa, kama mwanamke akiwa ni mtu wa madhila kwa mume basi mume huyo ataona kuwa hakuna haja ya kuishi tena duniani. Kwa msingi huu, mwanamke anapaswa kuwa mnyenyekevu, mpole na mtii

kwa mumewe kwa kila jambo atakaloambiwa. Inapotokea mwanamke akawa anapaza sauti yake juu ya ile ya mwanaume, anaweza kumfanya mwanaume huyo kutokuwa na raha ya kuishi duniani na kumsababishia kupata maradhi kama yale ya "Presha," kupanda au kushuka kwa mapigo ya moyo kuliko ilivyo kawaida. Kwa mfano, katika jamii za watu wa Libya mwanamke ni kiumbe ambaye anapaswa kumheshimu sana mume wake na mara nyingi hatakiwi kusema neno au kupinga jambo atakaloambiwa na mumewe mbele ya hadhara hata kama jambo hilo hakubaliani nalo. Hii inatokana na mafunzo ya dini ya Kiislamu ambayo yanaelekeza mwanamke kuwa hivyo.

Katika kitabu cha *Ashiki Kitabu Hiki* cha Shaaban Robert, pia kunaelezwa kuwa mwanamke ni kiumbe asiyetarajiwa kutoa lugha ya matusi. Anasema:

> Bi. Harusa na Bi. Chilli, wamejivunjia njia
> Wameingia mahali, huchukiza kuwaona
> Ya Rabi! Wape akili, hili wasitende tena
> Matukano si amali, hasa kwa wasichana (uk. 35).

Shaaban Robert anaonesha kuwa mwanamke kuzungumza lugha ya matusi ni kitu kibaya mno kupata kufanywa na mwanamke. Wataalamu wa masuala ya jinsia wanayaona maelezo kama haya yanatolewa na Shaaban Robert kuwa ni gandamizi na kumfanya mwanamke kujitoa kwa mwanaume (submissive to men) kwa kila jambo (Macknnon, 1991). Suala la kutotumia lugha ya matusi ni jambo ambalo linapaswa kutofanywa na watu wote katika jamii na si mwanamke peke yake. Hali hii inatokana na mfumo dume ambao si kwamba unamfanya mwanamke kuwa ni kiumbe mwema bali ni njia ya kumfanya asiwe na uwezo wa kuhoji au kuuliza jambo lolote kwa mumewe kwa kuwa kwa kufanya hivyo ataonekana anamdharau

mumewe. Mkazi mmoja wa eneo la Chumbageni alitueleza kuwa, tunaona inatokea katika jamii mtoto wa kike analazimishwa kuacha shule na kuolewa. Watoto wengi wa kike hushindwa kupinga na kulazimika kuolewa utotoni na kuacha shule. Hii inatokana na kunyamazishwa tangu wakiwa watoto wadogo kwa maelekezo kuwa mwanamke hatakiwi kujibizana na wazazi wake na hasa baba.

Mathias Mnyampala kwa upande wake, naye pia anamsawiri mwanamke kama kiumbe anayetakiwa kuwa mpole na mnyenyekevu kwa mwanaume. Mwanamke hatarajiwi kujibizana na mumewe kwa jambo lolote lile na anapokatazwa jambo lolote basi hutakiwa kuliacha mara moja. Kwa mfano katika ngonjera ya "Mke kuomba Ruhusa kwa Mume," anasema:

MKE
Nina jawabu adhimu, bwana nataka kwambia
Kuniradhi muadhamu, lazima kunisikia
Wala usinituhumu, kuwa bazazi wa njia
Nenda kwetu kutembea, niruhusu mume wangu

MUME
Jawabu yako naamu, Aziza sikuridhia
Walkalili fahamu, kwa ghadhabu kuniingia
Leo ni kutaramu, mengine wahitajia
Hwendi leo nakwambia, nikakaa peke yangu

MKE
Niruhusu tafadhali, jua nimeazimia
Nisirudie madhali, khasa nimekusudia
Bwana utanikatili, usiponikubalia
Nenda kwetu kutembea, niruhusu mume wangu

MUME
Ni bileshi kulalama, wala sitakusikia
Laaziza akirama, hayo uliyonambia
Na tena natuhuma, kuna dume langojea
Hwendi leo nakwambia, nikakaa peke yangu

MKE
Takwenda unifanyeni, lipi umekusudia?
Wewe ni mume gani, kama uliye nabiya?
Jama baba kanilani, kanipa chimvi balia
Nenda kwetu kutembea, niruhusu mume wangu (uk. 40-41).

Hapa tunaoneshwa majibizano baina ya mume na mke kuhusu mke kupatiwa ruhusa ya kwenda nyumbani kwao kumtazama dada yake. Kwanza, tunaoneshwa kuwa mwanamke hawezi kutoka nyumbani kwake kwenda mahali popote bila kutaka na kupatiwa ruhusa na mumewe. Mkazi mmoja wa Majengo katika Manispaa ya Dodoma anaeleza kuwa katika kabila lao la Wagogo ni wajibu wa mke kuomba ruhusa kwa mumewe pale anapotaka kwenda nje na nyumba yake na kutokufanya hivyo huhesabiwa kama ni utomvu wa nidhamu. Katika jambo lisilotegemewa mke anaonekana kubishana na mumewe kwa kulazimisha ruhusa ambayo mumewe amekataa kuitoa. Kwa kufanya hivyo, mwanamke huyu anamfanya mwanaume kuwa na mashaka kuwa huenda akiitoa ruhusa hiyo mkewe atakwenda kufanya maovu hasa yale ya zinaa.

Maelezo ya Shaaban Robert na yale ya Mathias Mnyampala yaliyotolewa hapo juu yanaonesha kufanana pale ambapo wote wanaonesha kuwa mwanamke hapaswi hata mara moja kubishana na mumewe juu ya jambo lolote kuhusu maisha yao ya ndoa. Badala yake mwanamke anapaswa kuitikia na kukubaliana na kila kitu anachoelezwa na mumewe. Tafauti ya msingi inayojitokeza kwa watunzi hawa wawili ni kuwa, Shaaban Robert ameonesha kutoa maonyo zaidi kwa mke kutothubutu kujibizana na mumewe hata siku moja. Analiona jambo hilo kuwa ni muongozo wa dini na unapaswa kuheshimiwa na atakayekiuka anapingana na mafunzo ya dini. Hii ndiyo hali iliyokuwepo wakati wa utunzi wa Shaaban Robert.

Kwa upande wake Mathias Mnyampala, anamuonesha mwanamke akibishana na mumewe bila taabu yoyote. Hii inaonesha kuwa katika kipindi cha Mathias Mnyampala tayari wanawake walishapiga hatua zaidi na kuanza kujibizana na waume zao. Kwa wataalamu wa masuala ya jinsia kama Ngaiza (2002) na Moore (1998) wanaiona hali hii kuwa ni hatua ya juu kabisa ya maendeleo kupata kufikiwa na wanawake katika harakati zao za kujikomboa. Mwanamke kupaza sauti yake na kupingana na baadhi ya mawazo ya wanaume ni ukombozi kutoka katika mfumo dume. Hatua hii itawafanya wanawake kuwa huru na kuamua kufanya mambo yao bila kuingiliwa na mtu yoyote. Si jambo la kubeza kwani hivi sasa wanawake wamekuwa na nafasi kubwa hata ya ushiriki katika katika nafasi za uongozi na kushiriki katika maamuzi yanayohusu maisha yao. Nafasi hii hawakuipata katika kipindi cha Shaaban Robert.

Hata hivyo, matatizo ya kuvunjika kwa ndoa yamekuwa mengi kwa sasa ikilinganishwa na ilivyokuwa katika miaka hamsini iliyopita (Ramadhan, 2013). Hii inaashiria kuwa kitendo cha wanawake kupata uhuru na nafasi kubwa ya kuweza kujibizana na waume zao kunaongeza migogoro mingi baina yao ikilinganishwa na kipindi ambacho wanawake hawakuwa na nafasi hiyo ya kujibizana na waume zao. Mtoto wa Shaaban Robert anayejulikana kwa jina la Iqbali Shaaban Robert alitueleza kuwa katika kipindi chote alichoshuhudia maisha ya baba na mama yake hakuwahi kumuona mama yake akijibizana na baba yake. Anasema: “mama alikuwa mtu mpole sana asiyependa kumuudhi baba kwa namna yoyote ile.” Hata hivyo, Moore (1998) anaiona hatua hii ya wanawake kupata nafasi ya kujibizana na waume zao ni hatua moja muhimu katika maendeleo ya masuala ya jinsia katika nchi za Afrika.

4.1.3 Mama na Malezi katika Jamii

Malezi ni hali ya wazazi au walezi kuwaongoza watoto wao katika misingi na maadili ya jamii yao. Momanyi (2001) anasema kuwa, jukumu la malezi ni la wazazi wawili (baba na mama) wa mtoto na si mmoja peke yake. Kutokana na mfumo dume uliopo katika jamii mama ndiye aliyeachiwa jukumu la kulea watoto na baba akishughulika na shughuli za uzalishaji mali na maendeleo kwa jumla. Hata hivyo, katika hali ya kushangaza mtoto anapokuwa na tabia nzuri za kusifika katika jamii, baba ndiye hupongezwa na kupatiwa sifa kwa malezi bora ya mtoto. Inapotokea mtoto huyo akawa na tabia isiyo nzuri ya kuridhisha, lawama za malezi mabovu humwangukia mama. Hii yote ni dalili ya mfumo dume ulioota mizizi katika jamii. Mathias Mnyampala anatuonesha kuwa jukumu la malezi kwa watoto si la mama pekee bali ni la wazazi wawili na jamii nzima kwa jumla. Tazama Shairi lake la "Maonyo kwa Mtoto," anasema:

> Ungamonya huu mwiko, mwiko kuushika moto
> Situme mkono wako, kushika kama kokoto
> Katu hutashika lako, hadi apate majuto
> Onyo lako kwa mtoto, kusikiwa ni katiti
> Kusikiwa ni katiti, aendapo batobato
> Na hasa ule wakati, wa uchanga na mtweto
> Mwendo anenda matiti, hajui mema mapito
> Onyo lako kwa mtoto, kusikiwa ni katiti
> Mwambie sishike wembe, wembe una mkeketo
> Kwa ulimi asilambe, tajikata zoloto
> Ataona kama embe, hadi akatwe mkato
> Onyo lako kwa mtoto, kusikiwa ni katiti (uk. 21).

Shairi hili linaanza kwa matumizi ya pili umoja kwa kumrejelea mtu fulani kuwa ndiye mwenye jukumu la kumuonya mtoto. Mtu huyu anaweza kuwa baba au mama kwa kuwa haikusemwa bayana ni nani hasa mwenye jukumu hilo. Kwa nukta hiyo, tunaweza kusema kuwa Mathias Mnyampala anaona kuwa wazazi wote wanalo

jukumu la kulea watoto wao. Mtoto anapopata malezi ya baba na mama huimarika zaidi kimadili na kimwenendo kuliko akilelewa na mzazi mmoja tu (Lyatuu, 2011). Kutokana na ukweli huo baadhi ya wazazi hulazimika kuishi pamoja hata kama ndoa yao ina misuguano mikubwa kwa nia ya kuwalea watoto wao wakiwa pamoja. Hawako tayari kuvunja ndoa zao kwa sababu wanafahamu wakifanya hivyo watasababisha watoto waishi bila ya malezi ya wawili hao.

Hata hivyo, tunaporejelea na kutazama shairi la "Maonyo kwa Mtoto," liliandikwa lini tunapata kubaini kuwa ni katika kipindi ambacho mwanamke ndiye aliyebebeshwa jukumu kubwa la kulea watoto na familia nzima. Hivyo, matumizi ya nafsi ya pili umoja katika msitari wa kwanza wa shairi, "Ungamwonya huu mwiko, mwiko kuushika moto," yanaashiria moja kwa moja kuwa aliyelengwa hapa ni mwanamke. Mwanamke ndiye aliyedhaniwa kuwa na jukumu la kulea watoto kwa sababu alikaa nao nyumbani siku nzima zaidi ya baba aliyeranda huku na huko kutafuta riziki.

Kimsingi, malezo yetu tuliyoyatoa hapo awali yanaonesha kuwa katika shairi la "Maonyo kwa Mtoto," mama na baba wote wanajukumu kubwa la kuwapatia watoto wao malezi bora. Kwa kutazama katika kipindi ambacho shairi hilo liliandikwa tukabaini kuwa anayelengwa katika malezi ya mtoto hapa ni mama zaidi kuliko baba. Upo usemi wa Kiswahili usemao, "Ukimwelimisha mama, umeelimisha jamii nzima." Usemi huu unatokana na hali halisi kuwa mama ndiye anayelea watoto nyumbani na kwa hiyo kutumia muda mwingi katika maisha yake akiwa na watoto. Kama kila mama akipata elimu juu ya malezi ya mtoto, itakuwa kazi rahisi kwake

kuwapatia watoto wake malezi bora. Hali ikiwa hivyo kwa akina mama wote ndivyo jamii nzima itakavyoelimika kutokana na mafunzo na maonyo ya mama.

Shaaban Robert kwa upande wake naye amezungumzia dhamira hii kwa kuonesha kuwa mwanamke wa zamani alikuwa na jukumu la kulea watoto na tena si mtoto mmoja bali watoto wengi. Katika *Insha na Mashairi* (1971) Anasema:

> Kinyume cha Mwanamke wa zamani. Aliyekuwa mtumwa na mtumishi wa kazi ngumu kama kibarua, Mwanamke wa zamani alionekana mchana na usiku nyumbani na jikoni, kuzaa na kulea umati wa watoto, Na mwenye lazima ya kufanya kazi ya kuangalia faraja za bwana: Mume wake.

Maelezo haya ni ushahidi tosha kuwa mwanamke alitazamwa kuwa ndiye mtu mwenye jukumu la kulea watoto na hakupatiwa msaada wowote katika hilo kutoka kwa mumewe na wanajamii kwa jumla. Kazi hii kwa hakika ni ngumu na haikuwa kazi pekee kwa mwanamke huyu. Wakati akilea watoto alipaswa pia kupika chakula, kufua nguo, kusafisha vyombo, kutafuta kuni na kwa ujumla kuhakikisha kila kitu katika familia kinakwenda sawasawa. Jambo kubwa na muhimu ambalo anatakiwa kufanya ni kuhakikisha kuwa mumewe anaishi maisha mazuri kabisa. Maelezo ya Shaaban Robert yanaonesha kuwa mwanamke anaelemewa sana na mzigo mkubwa wa kulea watoto. Kwa hili anaonesha kuwa na huruma kubwa kwa mwanamke.

Kwa maneno ya Shaaban Robert jukumu hili kubwa la malezi lilikuwa kwa mwanamke wa zamani. Maelezo yake tunakubaliana nayo kwa kuwa ni kweli kabisa mwanamke wa zamani alikuwa na jukumu kubwa la kulea watoto. Pamoja na ukweli huu, bado hata mwanamke wa siku hizi analo jukumu kubwa la malezi kwa watoto. Kwa mfano, mwanamke wa kijijini amezongwa na majukumu mengi katika familiya

yake na kubwa likiwa ni kulea watoto. Lyatuu (2011) anaeleza kuwa katika jamii ya watu wa vijijini, wengi wa wanaume wamesahau kabisa jukumu la kulea watoto na kuwaachia wanawake peke yao. Kila kitu mtoto atakachomuuliza baba yake, hujibiwa kuwa amuulize au amweleze mama yake na siyo yeye (baba).

4.1.4 Mwanamke na Suala la Uaminifu

Uaminifu ni kitu muhimu sana katika mahusiano ya mume na mke katika maisha yao ya kila siku. Uaminifu baina ya wawili hao ndio unaodumisha na kuendeleza mahusiano yao na kuyafanya kuwa mapya kila uchao (Ramadhani, 2013). Katika hali ya kawaida, uaminifu unapaswa kuwa watu wote katika jamii na si mtu mmoja peke yake. Hata hivyo, katika maisha ya siku hizi mwanamke anaonekana kulaumiwa kwa kukosa uaminifu na kusababisha matatizo makubwa katika jamii (Khalifa, 2013). Mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe laghai na mwenye kudanganyika kirahisi kwa ghilba na vitu vidogo kama vile fedha, mavazi, chakula na vitu vya aina hiyo na kumsaliti mwenzi wake. Shaaban Robert anaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe asiyemwaminifu na asiye aminika. Shairi “Kuoa,” lililopo katika *Pambo la Lugha* linasema:

> Kuoa mke wa haya, kukutazama hawezi
> Kama kweli yatakiwa, ni mke wa fumanizi
> Amwitaye humwendea, huwa hana kizuizi
> Na jambo hili li wazi, ya fahamu yasemwayo (uk. 18).

Hii inaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe asiye aminika hata kama akiwa na haya ya kutoweza kumtazama mtu usoni. Anaweza kuwa na haya kumtazama mumewe usoni lakini asiwe na haya ya kujizuia na uzinzi. Haya alizokuwa nazo mwanamke huyu ni za kinafiki tu na hazina ukweli wowote. Kwa nini haya alizonazo

mwanamke katika kumtazama mumewe zinapaswa kuwa hivyo hivyo katika mambo mengine ndiyo kuaminika kwa mwanamke huyo? Lakini anapokuwa na haya ya kumtazama mumewe usoni tu hana haya ya kuepuka zinaa na udanganyifu wa wanaume, mwanamke anakuwa ni kiumbe asiyeaminika.

Vile vile, hii inaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye hana uwezo wa kukataa maelezo yoyote anayoambiwa na mwanaume hata kama anayoambiwa yanaathiri maisha na ndoa yake. Mwanamke anafananishwa na mtoto mdogo. Anasema, “Amwitae huenda, huwa hana kizuizi.” Hii inamchora mwanamke kama kiumbe asiye na uwezo wa kutafakari jambo lolote analoambiwa na mtu yeyote bila ya kufikiria athari za hayo anayoambiwa. Mkazi mmoja wa barabara ya nane katika jiji la Tanga alieleza kuwa, mwanamke wa siku hizi ni mjanja asiyedanganyika kwa urahisi kama ilivyokuwa zamani. Habari ya kumdanganya mwanamke kwa Chips Kuku sasa imekwisha na wengi wa wanawake wanajitambua na wanajiheshimu.

Haya ni mawazo ya watu wenye mtazamo wa mfumo dume ambao humuona mwanaume kuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa wa kutafakari mambo kabla ya kufanya maamuzi. Kinyume chake, mwanamke hufanya maamuzi bila ya kufikiri na hujutia maamuzi yake baadae (Lyatuu, 2011). Huu ni ugandamizaji na udhalilishaji wa jinsia ya kike kwa kuwa si kweli kwamba wanawake wote hufanya maamuzi bila ya kufikiria. Wapo hata wanaume ambao wakati mwingine hujikuta wamefanya maamuzi bila ya kutafakari na kujutia baadae. Kufanya maamuzi yoyote yale bila ya kufikiria ni udhaifu wa kibinadamu na si wa mwanamke peke yake. Hivyo, si sawasawa kumlaumu mwanamke kwa makosa ambayo yanaweza kufanywa na mwanaume pia.

Mwanamke kiumbe ni asiye mwaminifu na asiyeaminika ni dhamira inayowasilishwa katika mashairi ya Mnyampala ya *Waadhi wa Ushairi* na *Ngonjera za Ukuta*. Katika shairi la "Mke Kuomba ruhusa kwa Mumewe," anasema:

> MKE
> Nina jawabu adhimu, bwana nataka kwambia
> Kuniradhi muadhamu, lazima kunisikia
> Wala usinituhumu, kuwa bazazi wa njia
> Nenda kwetu kutembea, niruhusu mume wangu
>
> MUME
> Jawabu yako naamu, Aziza sikuridhia
> Walkalili fahamu, kwa ghadhabu kuniingia
> Leo ni kutaramu, mengine wahitajia
> Hwendi leo nakwambia, nikakaa peke yangu (uk. 40).

Inaonekana mwanamke kunyimwa ruhusa ya kwenda kumtazama dada yake kwa kuhofiwa kwenda katika mambo ya ubazazi. Mwanamke mwenyewe tayari amekwishaweka shaka ya kukubaliwa ruhusa anayotaka ndiyo maana akatanguliza samahani kuwa yeye haendi katika mambo ya ubazazi bali anakwenda kumuona dada yake. Hii inaonesha kuwa, wanawake wamekwisha athiriwa na mfumo dume kiasi cha kujiona ni wakosaji kila mara. Pia, wanawake wamekwishaifahamu vizuri akili ya wanaume kuwa daima huwadhania kuwa ni watu waovu wasioaminika hata kidogo.

Shao (2004) anaona kuwa, wanawake ni watu ambao wameathiriwa sana na mfumo dume kiasi cha wao wenyewe kuendeleza unyanyasaji na ukandamizaji wa kijinsia dhidi yao wenyewe. Hii tunaiona pale mwanamke anapoomba ruhusa ya kutoka nyumbani kwa kujitetea kuwa haendi kushiriki katika mambo maovu. Kwa nini mwanamke huyo asiombe ruhusa bila ya kujitetea kuwa haendei mambo maovu? Ikiwa ataomba ruhusa bila kujitetea kuwa haendi kushiriki uovu, atapatiwa ruhusa

hiyo? Majibu ya maswali haya yanatupeleka katika ukweli kuwa mfumo dume umemfanya mwanamke kuonekana kama kiumbe asiyeaminika hata kidogo kwa mumewe na hata jamii kwa jumla. Tazama majibu ya mume kwa mkewe katika ubeti ufuatao:

> MUME
> Ni bileshi kulalama, wala sitakusikia
> Laaziza akirama, hayo uliyonambia
> Na tena natuhuma, **kuna dume langojea**
> Hwendi leo nakwambia, nikakaa peke yangu (uk. 41).

Mume ameamua kudhihirisha bayana kwa nini hataki kumpatia mkewe ruhusa ya kwenda kwao kutembea kwa msingi kuwa mkewe huyo ana miadi ya kukutana na mwanaume mwingine. Katika msitari wa tatu wa ubeti hapo juu maneno yaliyokozwa wino yanaashiria kuwa mwanamke huyo anakwenda kufanya zinaa na mwanaume asiye mumewe. Hali kama hii inajitokeza katika jamii nyingi duniani na si ya Waswahili peke yake. Kwa mfano, Katika nchi za Kiarabu, mwanamke hatakiwi kwenda mahali popote pale peke yake bila kuongozana na mumewe au ndugu yake wa kiume. Sababu kuu ya kufanya hivyo ni kumlinda mwanamke huyo asije akaingia katika maasi na wanaume wa barabarani. Pili, mwanamke ni kiumbe dhaifu ambaye hawezi kufanya maamuzi ya haraka akiwa peke yake na hivyo ni lazima awe na muongozo wa mwanaume. Tazama dondoo lifuatalo ambalo ni maelezo binafsi ya mtafiti:

> Wanafunzi wa kike kutoka katika nchi yangu ya Libya ambao wapo hapa Tanzania na kwingineko duniani wamefuatana na wanaume ambao ni ndugu zao wa karibu. Ndugu hao wanaweza kuwa ni kaka, baba, mjomba, babu, mtoto wa kiume wa kaka au dada. Ndugu huyo huandamana na mwanafunzi wa kike katika shughuli zote za masomo mpaka wanapomaliza. Ndugu wanaofuatana na wanafunzi hao wa kike

> hulipiwa gharama zote za maisha na serikali ya Libya katika kipindi chote hicho. Waarabu ni watu wenye wivu sana na wanawake na huamini kwamba, iwapo mwanamke ataachwa peke yake anaweza kuchukuliwa na wanaume wengine huko katika masomo yao. Pia, serikali ya Libya imepiga marufuku raia wake kuoa au kuolewa na mtu asiyekuwa Mlibya au Mwarabu kutoka katika mataifa ya Kiarabu yaliyoteuliwa.

Hii inaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe anayehitaji uongozi na ulinzi kutoka kwa mwanaume katika kila jambo analolifanya. Mwanamke peke yake hawezi kufanya mambo yakawa mazuri akiwa peke yake kwa kuwa hana uwezo huo. Mawazo haya si lolote wala chochote kwa wataalamu wa masuala ya jinsia kwani katika jamii wapo wanawake ambao hujiongoza wenyewe na hata kuongoza familia zao kwa manufaa makubwa. Koda (2000) anayaona mawazo kama haya kuwa ni njia ya kuimarisha makucha ya mfumo dume katika jamii.

4.1.5 Suala la Uasherati na Umalaya katika jamii

Uasherati na umalaya ni maneno yanatumika kumaanisha utendwaji wa tendo la ndoa pamoja na mambo yanayoambatana nayo pasipo halali ya kufanywa kwayo. Inapotokea mwanaume na mwanamke ambao si wanandoa kufanya ngono na yanayohusiana nayo huelezwa kuwa watu hawa ni Malaya au Asherati. Njogu na Wafula (2007) katika maelezo yao juu ya nadharia ya Ufeministi wanaeleza kuwa umalaya ni dhana anayopambwa nayo sana mwanamke katika jamii kuliko mwanaume hali ya kuwa wote wawili wanashiriki katika kadhia hiyo ya umalaya. Kutokana na mfumo dume ulioenea katika jamii wanawake wametupiwa kila jambo baya kuwa ni la kwao. Mathias Mnyampala anabainisha kuwa mwanaume na mwanamke ambao wanashiriki katika ngono isiyokuwa halali wote ni Malaya na asherati. Tazama beti zifuatazo kutoka shairi la “Malaya” katika *Waadhi wa Ushairi*:

Japo mtu wa silaha, machoni ukimuona
Amefunga na nikaha, yeye na mwana Amina
Ni mtu mwenye karaha, si mtu mwenye maana
Asherati hana haya, angawa mtu mkubwa

Na haoni mwanamke, po pote wakikutana
Lazima amtake, maneno yenyewe zina
Huzitoa pesa zake, mapenzi yapate fana
Asherati hana haya, angawa mtu mkubwa

Japo ni mke wa mtu, rafiki wanopendana
Kutongoza huthubutu, si kitu wakikosana
Huja uharibu utu, wanapofumaniana
Asherati hana haya, angawa mtu mkubwa (uk. 73).

Katika beti hizi tatu mtunzi anaonesha kuwa mwanaume ambaye tayari ana mkewe na mwanamke ambaye tayari ana mumewe nyumbani wanashiriki katika kitendo cha ngono kinyume na taratibu na kanuni za jamii. Kwa kauli hiyo, inaonekana kuwa Malaya anaweza kuwa mwanaume na mwanamke pia. Si vema kumlaumu mwanamke pekee kuwa ndiye Malaya na mwanaume akaachwa tu na wakati mwingine kupewa sifa nzuri kuwa yeye ni bingwa wa kufanya zinaa na wake za watu.

Katika ubeti wa tatu hapo juu mwanamke anasawiriwa kuwa ni kiumbe mpenda fedha na kutokana na hilo hughilibiwa na wanaume na kufanya nao zinaa hata kama tayari yeye ni mke wa mtu. Suala la wanawake kupenda fedha zisizopatikana kihalali ni jambo baya ambalo huwasababishia wanawake wengi kuingia katika mkondo wa maovu yenye madhara si kwao tu bali kwa wenzi wao, familia zao na jamii zao. Hata hivyo, anayetoa fedha hapa ni mwanaume kumpatia mwanamke ambaye ni mke wa mtu ili kumshawishi washiriki ngono. Mhojiwa mmoja wa eneo la Vibambani huko Tanga aliandika katika hojaji aliyopatiwa akihoji, kwa nini mwanamke ndiye

alaumiwe ati anapenda fedha kama kila mwanaume angelitunza fedha zake ni mwanamke yupi angelimlazimisha kumpatia. Kwa bahati nzuri katika jamii ya Watanzania na hata katika mataifa ya Kiarabu kama Libya, mwanaume ndiye mtongozaji huku mwanamke akiwa msikilizaji tu. Hakuna sababu yoyote ya mwanaume kutoa fedha kama anajiamini kuwa na ujuzi wa kutongoza. Kumbe mwanaume kutoa fedha kwa mwanamke kama kigezo cha kumpata mwanamke huyo ni udhaifu wa mwanaume kushindwa kutongoza kwa maneno.

4.2 Matumizi ya lugha ya Kisanaa katika Mashairi ya Washairi Teule

Matumizi ya lugha ni mojawapo kati ya mbinu nyingi za kisanaa zinazotumiwa na watunzi wa mashairi katika kusawiri dhamira katika kazi zao. Senkoro (1988) anaeleza kuwa matumizi ya lugha katika kazi ya ushairi ndiyo yanayowafanya watu kupenda au kutopenda kazi za mwandishi yeyote wa ushairi wa Kiswahili. Matumizi hayo ya lugha yapo ya aina kwa aina na huchaguliwa na mtunzi kulingana na ustadi alionao katika utunzi wa mashairi (Senkoro, 1988). Mtunzi bora wa mashairi ya Kiswahili husifika kwa ustadi wake katika uteuzi wa maneno ambayo yanalandana vizuri kwa vina na mizani (Masamba, 1983). Bila shaka huu ni mtazamo wa utunzi wa mashairi kwa mujibu wa wanamapokeo. Haijuzu, kwani Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ambao tunatafiti mashairi yao wote ni washairi wa Kimapokeo kwa maana ya kutunga mashairi yao kwa kuzingatia urari wa vina na mizani.

Pia, matumizi ya lugha ya kitamathali ndiyo hutawala kwa kiasi kikubwa katika lugha ya mashairi. Tamathali za semi zina sifa ya kufumba mambo na kueleza mambo mengi kwa muhtasari. Ushairi nao ni utanzu wa fasihi ambao hueleza mambo mengi lakini kwa kutumia lugha ya mkato, mnato na fumbizi kwa wasomaji

wake. Hivyo, mtu anapozungumza juu ya matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi hana tafauti na mtu anayezungumzia umuhimu wa maji ya bahari, mto au bwawa kwa samaki.

Washairi Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ni miongoni mwa washairi nguli wa mashairi ya Kiswahili ambao wanaheshimika sana kitaifa na kimataifa. Washairi hawa wanatumia lugha ya kitamathali katika mashairi yao kwa nia ya kufumba dhamira zenye maadili kuntu kwa jamii yao. Tamathali zinazotumiwa na watunzi hawa wawili ni takriri, tashibiha, taswira, sitiari, jazanda, kejeli, utani, majazi na nyinginezo.

4.2.1 Matumizi ya Takriri katika Mashairi ya Washairi teule

Njogu na Chimerah (2014) wanafasili takriri kuwa ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na watunzi wa mashairi kwa kurudirudia baadhi ya silabi, maneno na sentensi katika tungo zao ili kutoa msisitizo wa jambo ambalo wanadhani ni muhimu kwa wasomaji kulinasa mara moja. Matumizi ya takriri huifanya hadhira ya kazi ya ushairi kuwa makini na zingativu katika usomaji wao kutokana na nguvu ya takriri katika moyo wa msomaji. Senkoro (1988) anaiona takriri kama chombo kinachotumika katika kumkumbusha msomaji kile kilichosemwa katika ubeti uliotangulia na kuhusianisha na anachosoma katika ubeti ungalipo. Hii ni sawasawa na kusema kuwa matumizi ya takriri katika ushairi husaidia kuunganisha mawazo na kuleta mtiririko sahali kwa msomaji wa mashairi. Mathias Mnyampala katika shairi la “Mama,” lililopo katika *Waadhi wa Ushairi*, ametumia takriri za aina tatu zote kwa pamoja zikizungumzia nafasi ya mwanamke. Tazama mfano ufuatao:

Kama walipa fadhila, ya kushukuria wema
Na akubariki Mola, akujalie rehema
Jambo lenye na Jamala, mshukuru sana **mama**
Fadhila umpe **mama**, na Mola takubariki

Na Mungu takubariki, rehema utaichuma
Taichuma kwa Maliki, Muumba wetu Karima
Mama yu pekee baki, radhi ya **mama** ghanima
Fadhila umpe mama, na Mola takubariki

Fadhila **mama** umpe, na nyingi mno heshima
Yakupasa umlipe, pamoja nyingi huruma
Mwiko sana simtupe, ijapo ana kilema
Fadhila umpe **mama,** na Mola takubariki

Kama wataka mwamuzi, wa kuondoa zahama
Ya kuondoa ulozi, wenye ndweo na hasuma
Ni **mama** ndiye hirizi, wa kuondoa tuhuma
Fadhila umpe **mama**, na Mola takubariki

Beti hizo nne zinathibitisha matumizi ya takriri za aina tatu ambazo ni takriri silabi, takriri neno na takriri sentensi. Takriri silabi ni vina kati ambavyo vimekuwa vikibadilika kutoka ubeti mmoja na mwingine. Vina mwisho ni “ma” na vinafanana katika beti zote za shairi hapo juu. Takriri neno inajitokeza kupitia neno “mama” ambalo limerudiwa katika kila ubeti na zaidi ya mara moja katika baadhi ya beti. Neno hilo limerudiwa mara 8 katika shairi zima. Marudiorudio haya yanaifanya hadhira kuuona uzito wa mama katika jamii na hivyo kumpatia heshima anayostahili. Mama ndiye anayelea watoto kwa muda mrefu kuliko baba kwani mama huanza kazi hiyo ya ulezi tangu angali mjamzito na kuendelea na kazi hiyo ya ulezi kwa muda mrefu baada ya kuzaliwa mtoto huyo. Ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha kuwa analipa fadhila kwa mama yake kutokana na mengi aliyofanyiwa na mama yake. Takriri sentensi ndiyo inayokazia wazo hili, “fadhila umpe mama, na Mola takubariki.”

Shaaban Robert pia anayo matumizi ya takriri kama hizo katika mashairi yake. Kwa mfano katika Shairi la “Fedha,” lililopo katika *Ashiki Kitabu Hiki*, anasema:

> **Fedha** imevunja nguu,
> Milima ikatambaa,
> **Fedha** ni kitu Kikuu,
> Aliyenayo shujaa,
> Hutiiwa na wajuu,
> Wa chini wakaridhia.
>
> Mtu aliye na **fedha**,
> Japo duni ni kubeli,
> Asemalo lina ladha,
> Neno lake Ikibali,
> Hazukiwi na bugudha,
> Uongowe huwa kweli (uk. 8-9).

Neno “fedha,” katika beti hizi mbili limerudiwa mara tatu zaidi kuliko maneno mengine yaliyopo katika beti hizo. Kurudiwarudiwa kwa neno hilo kunatoa msisitizo kwamba fedha huweza kutumika kufanya jambo lolote zuri na baya katika jamii. Kwa mfano, fedha huweza kutenganisha au kuvunja ndoa ya mtu. Kwa mfano, hutokea katika jamii mke kumuacha mumewe na kwenda kuolewa na mwanaume mwingine kwa sababu ana fedha na yule mume wa kwanza ni masikini. Vile vile, vitendo vya umalaya na uasherati vinavyofanyika katika jamii na lawama kubwa ikielekezwa kwa mwanamke ni ishara tosha ya kwamba fedha ndiyo zinazosababisha mambo haya kutokea katika jamii.

Washairi wote wawili wana matumizi ya takriri katika mashairi yao. Takriri zilizotumika zina nia ya kusisitiza juu ya mambo ya msingi ambayo mtunzi anataka hadhira yake iyapate. Mathias Mnyampala anaonekana kuwa na matumizi ya takriri neno mara nyingi zaidi kuliko Shaaban Robert. Kwa mfano, Mathias Mnyampala amerudia takriri neno “mama” mara nane katika shairi la “Mama,” wakati Shaaban

Robert amerudia neno “fedha,” katika shairi la “Fedha” mara tatu tu. Hii ni kwa mujibu wa mifano iliyopo hapo juu. Pia, Mathias Mnyampala amekuwa na matumizi ya takriri sentensi katika shairi la “Mama” tulilolitolea mfano hapo juu hali ya kuwa Shaaban Robert hakuonesha matumizi hayo katika shairi la “Fedha” tulilolitolea mfano hapo juu. Hata hivyo, wote kwa pamoja wameonesha kuwa matumizi ya takriri za aina kwa aina ni muhimu katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira ya mashairi.

4.2.2 Matumizi ya Tashibiha katika Mashairi ya Washairi Teule

Tashibiha ni tamathali za usemi ambazo hutumika kulinganisha vitu vyenye sifa na tabia tofauti kuwa ni kitu kimoja chenye kufanana bila ya kutofautiana (Njogu na Chimerah, 1999). Tashibiha hutumia maneno ya mlinganisho kama; sawasawa na, mithili ya, kama, anafanana na, na mfano wa. Matumizi ya maneno haya ya ulinganisho hutupatia tashibiha ambazo huiwezesha hadhira kupata dhamira zilizomo katika shairi hilo. Shaaban Robert katika shairi “kuoa,” lililopo katika *Ashiki Kitabu* Hiki anasema:

> Kuoa mke si kufu,
> Atakuliza machozi,
> Kwa mambo yake dhaifu,
> Ukonde ubaki ngozi,
> Huwezi kumsarifu,
> Cheo chako hakiwazi,
> Kwake kama upuuzi,
> Yafahamu yasemwayo (uk. 6).

Hapa tunaoneshwa matumizi ya tashibiha “Ukonde ubaki ngozi,” yakifafanua vizuri dhamira ya ya mateso ya mwanaume kutoka kwa mkewe. Shaaban Robert anafunza kuwa kuoa si jambo la kupapiapapia na kukimbilia kwani madhara yatokanayo na

matatizo ya ndoa ni makubwa. Kabla ya kuoa mtu anatakiwa kufanya utafiti wa kina juu ya mchumba wake kwa nia ya kujiridhisha kuwa atakuwa mwenza sahihi kwake. Pasipo kufanya utafiti kabla ya kuoa na kuamua kuoa mwanamke yeyote tu kunaleta matatizo ya mwanaume kukonda na kubakia kama ngozi. Hii ina maana kwamba kutokana na kero za mke asiyekuwa mwema kwa mumewe, humfanya mumewe huyo kuwa na hali mbaya kiafya kutokana na mawazo. Hii inawataka watu wote kuwa makini katika kutafuta mwenzi wa kumuoa au kuolewa.

Mjadala katika aya ya hapo juu unaonesha kuwa mwanamke ndiye mtu anayeweza kusababisha matatizo kwa mume na katika ndoa kwa jumla. Huu ndio mtazamo wa watu wengi katika jamii kiasi hata cha kuwakataza watoto wao wa kiume wasioe binti kutoka nyumba fulani kwa madai kuwa watoto wa nyumba hiyo ni watovu wa adabu. Hili kwa hakika ni eneo mojawapo kati ya maeneo makubwa ya ugandamizaji wa jinsia ya kike (Khalifa, 2012). Si kweli kuwa wanawake ndiyo watu wabaya wasababishao matatizo katika familia na kuwakondesha waume zao. Ni baadhi tu ya wanawake ndiyo huwa na tabia mbaya katika ndoa kama ilivyo pia kwa baadhi ya wanaume. Katika ngonjera ya “Maana yake nini Nyama ya Ulimi,” Mathias Mnyampala anasema:

JAWABU

Ni maneno ya ufumbe, yatakiwa kufumbua
Ya usemi wa vijembe, ukweliwe hupindua
Ni maneno ya ubembe, mjinga kumzindua
Maneno ya kuzindua, ndiyo nyama ya ulimi

Kiutumia vizuri, mambo takuwa fahua
Ulimi taleta heri, kwa mapenzi ya murua
Ulimi kileta shari, ndiyo shari tavumbua
Maneno ya kuzindua ndiyo nyama ya ulimi

Ulimi waponza Kichwa, kwa maneno kufyatua
Halijazama likachwa, huja kuzua belua
Aso jeuri huachwa, **hupendwa kama halua**
Maneno ya kuzindua, ndiyo nyama ya ulimi

Mtu kumridhi mke, mpe neno la murua
Japo awe na makeke, wazimu utapungua
Neno jema utamke, mwelewa hupata afua
Maneno ya kuzindua, ndiyo nyama ya ulimi (uk. 85).

Sehemu ya ngonjera hii ya Mathias Mnyampala ina matumizi ya tashibiha **hupendwa kama halua**. Hii ina maana kuwa mwanamke ambaye si msemaji sana wa maneno hupendwa na mumewe pasina kifani. Mke wa mtu hapaswi kuwa mtu wa vijembe kwa mumewe na kwa watu baki katika jamii. Mwanamke anapaswa kuwa mtu mpole na heshima asiye na sauti ya juu kwa mumewe. Hii itamfanya mke huyo apendwe na mumewe kwa upendo usio kifani kama vile watu wanavyopenda halua. Halua ni aina ya kitafunwa kitamu mno kinachotengenezwa kwa nafaka, viungo, sukari na mafuta.

Katika ubeti wa nne kunaoneshwa kuwa, mwanaume naye anapaswa kuwa mtuvu wa ulimi kwa mkewe. Mwanaume hapaswi kuwa na lugha ya masimango na kero kwa mkewe kwani atasababisha kuchukiwa na mkewe. Kumbe si mwanamke peke yake ambaye anatakiwa kuwa na maneno laini na ukarimu kwa mumewe hata mwanaume pia anapaswa kuwa hivyo hivyo kwa mkewe. Wana nadharia ya Ufeministi kama Moore (1998) wanaiona hali kama hii kuwa ni hatua ya juu ya maendeleo kufikiwa katika harakati za ukombozi wa wanawake kutoka katika makucha ya mfumo dume. Mfumo dume uliwafanya wanawake kuwa chini na kujinyenyekeza kwa waume zao huku wanaume wakionekana kuwa katika tabaka la juu la kuwanyanyasa wanawake.

4.2.3 Matumizi ya Taswira katika Mashairi ya Washairi Teule

Taswira ni picha anayoipata msomaji wa ushairi baada ya kusoma shairi ambalo limepambwa kwa lugha ya mafumbo. Senkoro (1988) anaeleza kuwa taswira ni maneno ambayo yalivyopangwa katika shairi huweza kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au mawazo mengine. Tunajifunza kuwa taswira hujitokeza akilini kwa msomaji wa shairi kwa sababu ni katika mashairi ndiyo kuna matumizi makubwa ya taswira kuliko ilivyo katika kazi nyingine za fasihi. Shaaban Robert katika shairi la "Sijui," ndani ya diwani ya *Ashiki Kitabu Hiki* anaeleza:

> Mwanamume kinyozi,
> Dada mimi simwezi,
> Heri nipande ngazi,
> Nende japo kwa goa.
>
> Sinifanyie kelele,
> Maneno mapesa mbele,
> Nikanunue mchele,
> Huko nitakofika (uk. 12).

Taswira ya haraka haraka inayopatikana katika shairi hili ni kuwa mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe anayependa fedha zaidi kuliko kitu kingine katika maisha. Kutokana na kupenda kwake fedha amekuwa ni mtu asiyekuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe. Mwanamke wa aina hii yupo tayari kumwacha au kumsaliti mumewe kwa kufanya ngono na wanaume wengine wenye fedha.

Katika shairi la "Sinyamaziki" katika kitabu cha *Mwafrika Aimba* cha Shaaban Robert tunapewa taswira nyingine inayohusu nafasi ya mwanamke kwa mumewe. Tazama mfamo:

> Sana nilimnyenyekea,
> Bali sikupata wema,
> Mali imenipotea,

Ndipo nikarudu nyuma,
Na sasa najijutia,
Nikikumbuka gharama,
Sinyamaziki kusema-
Hukumbuka mali yangu.

Huba ilinikithiri,
Moyo na mwili mzima,
Miliki nikahasiri,
Kuuza chini ya kima,
Fedha nimpe mzuri,
Anisabilie wema,
Sinyamaziki kusema-
Hukumbuka mali yangu.

Nilitoa kwa mapenzi,
Nipate njema hatima.
Hakuuweza ulezi,
Akanitupa yatima.
Sasa sina usingizi,
Machoni umenibana.
Sinyamaziki kusema-
Hukumbuka mali yangu (uk. 13-14).

Beti hizi za shairi zinaonesha taswira kuwa, mwanaume alifanya kila aliloweza kumridhisha mkewe lakini mkewe huyo alimuacha mumewe na kuondoka zake. Mume amepatwa na simanzi kubwa na hata kuanza kujutia mali zake alizotumia katika kumridhisha mkewe na sasa ameyoyomea kwingine. Hii inathibitisha msemo wa Waswahili, “fedha siyo kila kitu katika maisha.” Mtu anaweza kuwa na fedha na mali nyingi lakini akakosa raha na amani katika maisha yake na fedha zake zisimsaidie kitu.

Mathias Mnyampala anatupatia taswira ya umuhimu wa mzazi au wazazi kuwajali watoto wao kwa kuwapatia mahitaji yao yote ya msingi katika maisha. Katika shairi la “Kuku,” lilipo katika *Waadhi wa Ushairi* anasema:

> Akose kinywa na kucha, haachi kutabaruku
> Watotowe hataacha, Vifaranga vyake kuku
> Akichokozwa huchacha, kishikwa na dukuduku
> Mfano huo wa kuku, hufatwa na kila chumbe (uk. 3).

Ubeti huu unatupatia taswira kamili ya mzazi hasa mama alivyo na huruma kwa wanawe. Daima, kuku huwa hawaachi watoto wake mbali na alipo yeye kwa kuhofia kudhuriwa na maadui kama mwewe na wanyama wengine hatari kwa maisha ya vifaranga ambao ni kuku wa baadae. Hii inafanana sana na mama ambapo siku zote huwa karibu na watoto wake popote anapokwenda. Katika nchi zenye vita akina mama hupata taabu kubwa ya kukimbia mashambulizi kwa sababu hulazimika kukimbia wakiwa na watoto mgongoni na wengine wadogo mikononi. Hii huwafanya kukosa kasi ya kukimbia mashambulizi na kuuwawa pamoja na watoto wao.

Msitari wa mwisho katika ubeti wa shairi hapo juu unaonesha kuwa mfano wa kuku kujali na kuthamini watoto wake hufuatwa na kila kiumbe. Katika uhalisia, mfano huu hufuatwa na wanawake kuliko wanaume. Baadhi ya wanaume hutelekeza familia zao na kuwacha wanawake wakiteseka kuwapatia watoto mahitaji ya maisha (Ngaiza, 2004; Koda, 2000). Hii inatokana na dhana ya kwamba mwanamke ndiye mwenye jukumu la kulea watoto na baba ana jukumu la kutafuta mahitaji ya kujikimu kimaisha. Inapotokea baba ameshindwa kupata mahiyaji hayo huikimbia familia yake na kumwachia mama mzigo huo mkubwa. Madhumuni ya Mathias Mnyampala kutoa msitari huo ni kutoa mawaidha kwa wanajamii wote kuiga mfano wa kuku katika malezi ya watoto na si kumwachia mama peke yake. Mara nyingi taswira hukaribiana sana na ishara na kwa hiyo ni vema tutazame tamathali ya ishara inavyojitokeza katika mashairi ya washairi teule.

4.2.4 Ishara katika Mashairi ya Washairi Teule

Tamathali ya usemi aina ya Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali anayotumia msanii katika kazi yake ya fasihi kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine (Senkoro, 1988). Mathalani, katika shairi la Abdilatif Abdalla la "Mnazi: Vuta N'kuvute" katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*, mshairi katika kuzisawiri hali za uchumi na kisiasa zilivyo Afrika ametumia taswira ya mnazi na walanzi, ambayo ni sihara ya mvutano uliopo baina ya akina ALII na BADI (Senkoro, ameshatajwa). Maelezo haya yanatupatia ufahamu kuwa, washairi hutumia vitu halisia katika jamii kujenga ishara ambazo ndani mwake mna dhamira za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Shaaban Robert katika shairi lake la "Nyumba za Ngoma" anasema:

> Wanawake magunge,
> Wamezidi pangapunge,
> Heri tusiwahonge,
> Wataka kutuibia (uk. 13).

Ubeti huu unatoa ishara kuwa wanawake wanaendekeza sana vitendo vya umalaya na ukahaba katika jamii kwa ajili ya kujipatia kipato. Hii inaonesha kuwa umalaya na uasherati vimekuwa ni vitu vya kawaida katika jamii. Mshairi anaonesha pia wanaume ndio wanaochangia katika kuendeleza vitendo vya umalaya na ukahaba katika jamii kutokana na kuwahonga wanawake fedha ili wakubaliane kufanya tendo hilo. Kama wanaume wangekuwa na msimamo wa kutowahonga wanawake ili kununua ngono, umalaya na ukahaba usingelikuwapo kwa kasi kubwa katika jamii. Haya ni mawaidha anayoyatoa Shaaban Robert kwa wanaume kama njia ya kupunguza vitendo vya umalaya na ukahaba katika jamii.

Katika Shairi lake jingine la “Nani atakutendea?” ametoa ishara ya ushauri na mawaidha kwa wanawake nao kutokubali kurubuniwa na wanaume kushiriki katika ngono zisizo na utaratibu unaotambulikana. Anasema:

> Na wanaume magunge
> Wamezidi pangapunge
> Kina dada tujitenge
> Hasara itatujia (uk. 14).

Hii inatoa ishara kuwa si vema kutoa lawama kwa wanawake peke yao kuwa ni Malaya na asherati na kuwasahau wanaume. Wanaume ni wadau muhimu katika kuendeleza au kupunguza vitendo vya umalaya katika jamii. Hii ni kwa sababu umalaya na ukahaba hauwezi kufanywa na mwanamke peke yake bila ya kuwapo mwanaume. Kwa ubeti huu, Shaaban Robert anatoa mawaidha kwa wanawake kukataa kudanganywa na wanaume kwa fedha na kukubali kushiriki ngono zitakazo hatarisha maisha yao.

Mathias Mnyampala kwa upande wake naye pia ametumia tamathali ya usemi ya ishara kuwasilisha dhamira zinazohusu masuala ya jinsia baina ya wanaume na wanawake. Katika shairi la “Ubaya” Lilipo katika *Waadhi wa Ushairi*, anasema:

> Nyoka hujiviringisha, akaingia shimoni
> Njiani hujiepusha, kukimbia hatarini
> Lakini mwovu komesha, akikuuma huponi
> Mwovu huwa hajioni, husingizia wengine
>
> Husingizia wengine, kujitoa nuksani
> Ubaya wake akane, akajiweka pembeni
> Usiku akugugune, akutoe duniani
> Mwovu huwa hajioni, husingizia wengine
>
> Ubaya hauna kwao, tangu pembeni pembezoni
> Po pote una kikao, tangu hapa na mwishoni
> Kwa kila wautakao, hauwatoki maishani
> Mwovu huwa hajioni, husingizia wengine (uk. 11-12).

Katika beti hizo tatu, mshairi anatoa ishara ya ubaya katika jamii kwa kumtumia nyoka ambaye huuma watu na kujificha katika shimo akihofia kuuwawa na watu. Hii ni ishara ya mtu yeyote mwovu katika jamii kwani anapofanya uovu hujificha ili watu wasimuone. Mtu huyu anaweza kuwa mwanaume au mwanamke. Kwa mfano, mke wa mtu anaweza kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanaume mwingine nje ya ndoa yake na akawa anakutana kwa siri kubwa na mwanaume huyo. Hufikia mahali mume na hawara wa mke wakakalishwa meza moja na kula chakula bila ya kutambuana. Huu ndiyo ubaya wa mwanamke unaofananishwa na ule wa nyoka kuuma watu na kukimbilia shimoni. Mfano kama huu unaweza pia kumwangukia mwanaume ambaye tayari ana ndoa au ana mpenzi wake wa kudumu lakini anatoka nje ya mahusiano hayo. Simu ya nyoka ni kali na huweza kusababisha kifo kwa aliyeumwa na nyoka. Hii ni sawasawa na mwanaume au mwanamke kutoka nje ya ndoa na kuukwaa UKIMWI. UKIMWI ni zaidi ya kuumwa na nyoka kwani una hatari kubwa katika maisha ya mwanadamu.

Matumizi ya lugha ya kisanaa katika kazi za fasihi ni uwanja mpana ambao hauwezi kutafitiwa katika utafiti huu na kumalizika. Si tu katika utafiti huu, hata katika utafiti wowote ule unaohusu fasihi ya Kiswahili ni vigumu kwa mtafiti kutafiti vipengele vyote vya lugha ya kisanaa na kuvimaliza vyote. Vipengele vya matumizi ya takriri, tashibiha, taswira na ishara vilivyowasilishwa katika utafiti huu vimeweza kutuwezesha kukamilisha dhumuni mahususi la pili la utafiti huu. Kwa kutumia vipengele hivi, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wameweka bayana nafasi ya mwanamke katika jamii sambamba na ile ya mwanaume. Kwa jumla, washairi hawa wawili wanaonekana kutumia lugha ya kuwaidhi zaidi juu ya wanawake na wanaume

kuacha kutenda mabaya na kuwa watu wema. Mwanamke anasawiriwa kuwa na nafasi ya juu kabisa katika ulezi wa watoto tafauti na ilivyo kwa baba. Wataalamu wa masuala ya jinsia wanaiona hali hii kama ukandamizaji wa jinsia ya kike unaofanywa na wanaume kupitia mfumo dume uliopo katika jamii. Sambamba na hilo, washairi hawa wawili wameonesha pia mwanaume analo jukumu kubwa la malezi kwa mtoto na asimwachie mkewe kazi hiyo yeye mwenyewe.

4.3 Falsafa ya Washairi Teule Juu ya Mwanamke

Falsafa kuhusu maisha hutafautiana kutoka mtunzi mmoja na mwingine na baadhi hufanana. Wahakiki waliohakiki kazi za Kezilahabi kama Frolova (2003) anasema kuwa kazi hizo zinatoa mkondo wa kifalsafa unaoyaona maisha kuwa hayana maana. Waliohakiki kazi za Shaaban Robert kama Senkoro (1988) anaziona kazi hizo kuwa zinayaona maisha kuwa na maana kubwa kwa mwanadamu. Hii ndiyo tafauti ya falsafa iliyopo baina ya waandishi kuhusu maisha. Ili kutimiza madhumuni mahususi ya tatu ya utafiti huu tutaanza kwa kutafiti falsafa ya maisha katika mashairi ya Shaaban Robert na baadae mashairi ya Mathias Mnyampala.

4.3.1 Falsafa ya Shaaban Robert juu ya Mwanamke

Shaaban Robert anamuona mwanamke kuwa na nafasi kubwa katika kuyafanya maisha ya duniani kuwa mazuri au mabaya. Mwanaume aliyejaaliwa kupata mke mzuri huishi maisha kama ya peponi. Yule aliyejaaliwa kupata mke mwovu na msumbufu huishi maisha mabaya ya shida na taabu kama aliye motoni. Falsafa hii inatokana na mafundisho ya dini ya Kiislamu kwamba mwanamke ni kiumbe wa kumtumikia mume kwa kumstarehesha kwa starehe mbalimbali za Kibailojia, kijamii

na kiutamaduni. Katika shairi la “Dunia Njema” katika kitabu cha *Ashiki Kitabu Hiki* anasema:

> Dunia nzuri na mambo yake,
> Yana fahari ya peke yake,
> Juu sayari ni taa zake,
> Chini Johari ardhi yake.
> Zulia lake nyasi kijani,
> Na maji yake mvua mbinguni,
> Kushuka kwake milele shani,
> Sifa ni zake Mola Manani (uk. 28).

Hii inamaanisha kuwa dunia ni mahali pazuri pa kuishi na kupata starehe za aina kwa aina kutokana na mambo ya dunia. Msitari wa kwanza wa ubeti huu unajenga ishara kuwa kinachoifanya dunia kuwa mahali pazuri pa kuishi ni mambo yake. Mambo haya ni pamoja na kuwa na mke mwema na mwadilifu. Tumeihusianisha ishara hii na shairi la “Kuoa” katika diwani hiyohiyo ambalo linaeleza kuwa:

> Kuoa mke si kufu,
> Atakuliza machozi,
> Kwa mambo yake dhaifu,
> Ukonde ubaki ngozi,
> Huwezi kumsarifu,
> Cheo chako hakiwazi,
> Kwake kama upuuzi,
> Yafahamu yasemwayo (uk. 6).

Hii inamaanisha kuwa kuoa mwanamke ambaye ni muovu na asiye na adabu ni dhiki kubwa katika maisha ya mwanaume. Kumbe starehe kubwa katika maisha ya mwanaume ni kuwa na mke mwema. Ili kuepukana na dhiki hii Shaaban Robert anawataka wanaume kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu kuomba kupatiwa mke mwema. Mwanamke watakaye muomba kutoka kwa Mwenyezi Mungu awe amepambika kwa sifa nzuri. Miongoni mwa sifa hizo ni zile zilizopo katika shairi la “Urafiki” katika kitabu cha *Pambo la Lugha*. Anasema;

Umbo la kupendeza, kama la malaika
Sura ya kufurahisha, kama ile ya pepo
Umbo la takaso, kama mbingu na mwezi
Hulingani na mkadi, labda luli bahari (uk. 32).

Huyu ndiye mwanamke ambaye Shaaban Robert anamuona kuwa ataweza kumpatia mwanaume starehe ya duniani. Momanyi (2001) anaziona sifa alizopambwa mwanamke katika ubeti huu ni za kumfanya kuwa ni kifaa cha kutumiwa na mwanaume kama chombo cha starehe. Momanyi (ameshatajwa) amesahau kuwa Falsafa ya Shaaban Robert kumhusu mwanamke ni kuwa, ni kazi na wajibu wa mwanamke kumpatia mumewe starehe zote anazohitaji katika maisha. Hata hivyo, tunapingana na mawazo ya shaaban Robert hapo juu kuwa sifa alizompamba nazo mwanamke katika ubeti hapo juu hazitoshi kumfanya mwanamke kuwa kiumbe anayeweza kumpatia mwanaume starehe zote anazohitaji katika maisha. Sifa muhimu aliyoisahau katika ubeti huu ni tabia njema ya mwanamke. Mwanamke muovu atamfanya mumewe kuwa mtu wa shida na taabu katika maisha yake yote.

Katika kuendeleza falsafa yake kuhusu nafasi ya mwanamke katika maisha ya mume na jamii kwa jumla, Shaaban Robert anaonya kuwa starehe hizo huwa zina mwisho wake. Katika Shairi la “Maswali na Majibu” katika *Ashiki Kitabu Hiki* anasema:

Dunia imetubana,
Imetuvika masombo,
Tulikwenda kwa mapana,
Tukapiga watu fimbo.
Ngoma ikivuma sana,
Ni kupasuka kiwambo,
Roho zimejaa mambo,
Radha ziko wapi tena? (uk. 105).

Hii inaonesha kuwa starehe anazopata mwanadamu hapa duniani ikiwamo ile ya kuwa na mke mwema na kushiriki naye katika starehe za kingono, hufika mahali

zikaisha. Kwa sababu starehe hizo huwa zinakwisha mwanadamu anaaswa kutoziabudu na kuziendekeza starehe hizo. Kutokana na kuendekeza starehe hizo baadhi ya watu hutoka nje ya ndoa zao na kujisababishia madhara makubwa ya kupata maradhi. Pamoja na Shaaban Robert kuonesha falsafa yake juu ya mwanamke kuwa na nafasi kubwa katika kumpatia mwanaume starehe za dunia ametoa pia hadhari muhimu kwa wanaume kutoendekeza starehe hizo na kufikia kufanya maasi. Hadhari hii ni sahihi na inapendeza ikifuatwa na wanajamii katika maisha yao ya kila siku. Baadhi ya wanaume wanapoona wake zao wamezeeka hutafuta watoto wadogo wa kike na kuwa na mahusiano nao.

Kwa upande wa pili falsafa ya Shaaban Robert kumhusu mwanamke inaona kuwa mwanamke anapaswa kupata stahili sawa na zile anazopata mwanaume katika maslahi ya kazi. Haiwezekani mwanamke na mwanaume wakafanya kazi iliyo sawasawa halafu mwanamke akapata ujira kidogo na mwanaume ujira mkubwa. Kwa mfano, wakati mwanaume anakwenda kazini asubuhi mwanamke hubaki nyumbani kulea watoto wao na kufanya kazi za ndani kama kufua nguo, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, kuandaa chakula na kuwahudumia watu wote waliopo katika nyumba yao. Kazi hizi huwa hazina malipo kwa mwanamke na hata akiwa na shida yoyote ile inayohitaji kutatuliwa kwa fedha inakuwa vigumu kuitatua. Mwanaume ambaye amemwachia mke mzigo mzito wa shughuli nyumbani hulipwa mshahara na hathubutu hata mara moja kumkumbuka mke ambaye ndio anayeandaa mazingira mazuri ya mume kufanya kazi. Katika shairi la “Nani Atakutendea” anaeleza:

Kazi bila manufaa,
Nani atakutendea,
Sinifanyie hadaa,
Kungwi hakunihusia.

Sinifanyie hamaki,
Shetani wangu hataki,
Sharti unipe haki,
Ndipo ataputulia (uk. 13).

Shairi hili linaonya kuwatumikisha wanawake kwa kazi nyingi bila ya kuwapatia malipo stahiki au hata kutambua mchango wao. Usawa wa malipo baina ya mwanaume na mwanamke katika kazi ni kitu muhimu kitakacholeta ustawi wa maisha ya wanaadamu wote katika maisha yao ya duniani.

4.3.2 Falsafa ya Mathias Mnyampala juu ya Mwanamke

Mathias Mnyampala ana fanana na Shaaban Robert juu ya falsafa ya maisha kumhusu mwanamke. Anamuona mwanamke kuwa ni kiumbe muhimu katika kumsaidia mwanaume kutimiza majukumu yake. Haya yanabainika katika shairi "Taji la Nyumba" kwa mfano:

Taji kitu cha heshima, avae vema mvaaji,
Atulizane mtima, kama mtungi na maji,
Si vae mwenye kilema, hawi huyo mtunzaji,
Mke mwema ndiye taji, la utukufu wa mumewe.

Taji lipambiwe zari, zaujati na zauji,
Mume ni bwana shauri, kwa jamii mtunzaji,
Taji hili la fahari, nyumbani linafariji,
Mume mwema ndiye taji, la utuvu wa mkewe.

Asiye heshima mke, atakuwa mfujaji,
Hata pia mume wake, akiwa mkorogaji,
Na taji lisichafuke, kwa mambo ya ulewaji,
Mume na mke ni taji, la utukufu wa nyumba (uk. 11).

Hii inamaanisha kuwa mwanamke ana nafasi kubwa katika kuyaimarisha maisha ya mumewe. Mwanamke akiwa mtu mwema kwa mumewe, mume huyo atapata raha isiyokifani katika maisha yake. Katika ubeti wa kwanza msitari wa kwanza

tunaelezwa sifa za taji na kazi zake. Taji huvikwa mtu aliyepata mafanikio maalumu kama ishara ya kumpongeza kwa mafanikio yake. Mwanamke kufananishwa na taji ni sawa na kusema kwamba muonekano wa mume ulivyo hufanywa na mke. Kama mume ni nadhifu na mwenye furaha, ni zao la mke katika jitihada za kumnawirisha mume wake. Na kama mume ni mkondefu, asiye na furaha na mchafu pia ni zao la mke wake. Hili linapatikana katika msitari wa mwisho wa ubeti wa kwanza, “mke mwema ndiye taji la utukufu wa mume.”

Mathias Mnyampala hakuwa na upendeleo katika falsafa yake juu ya nafasi ya mwanamke katika jamii na kwa mumewe. Katika ubeti wa pili anaonesha kuwa, ili mwanamke aweze kumfanya mumewe kuwa na utukufu katika jamii ni lazima apate ushirikiano kutoka kwa mumewe. Mume ndiye ambaye atamfanya mkewe afanye kazi za kumnawirisha na kumfanya mumewe kuwa na utukufu katika jamii. Mwanamke anahitaji utulivu wa nafsi ili kuweza kumhudumia mumewe. Utulivu huo wa nafsi kwa mke utapatikana kama mwanaume atampenda mkewe na kutomsaliti kwa kutembea na wanawake wengine nje ya ndoa yao. Katika ubeti wa mwisho wa shairi la “Taji la Nyumba” kunatolewa msisitizo kuwa ustawi wa familia ni mume na mke wote kuwa watu wema. Si mke au mume peke yake anayeweza kujenga ustawi katika maisha bali wote wawili.

4.3.3 Hitimisho

Kwa jumla Shaaban Robert na Mathias wanaonekana kutawaliwa na mawazo ya mfumo dume katika kumsawiri mwanamke. Falsafa zao zinamtazama mwanamke kama kiumbe asiyeaminika na msaliti katika maisha ya ndoa. Mwanamke anasawiriwa kuwa ni kiumbe anayependa fedha na huweza kufanya jambo lolote

baya kwa ajili ya kujipatia fedha. Haya yanaonekana pale wanapomsawiri mwanamke kama kiumbe Malaya na kahaba anayeendekeza vitendo vya kiasherati. Kwa kiasi kidogo mwanaume naye amesawiriwa kujihusisha na vitendo hivyo vya umalaya na uasherati. Tulidhani ingekuwa vema mwanaume akasawiriwa kuwa ndiye anayeoongoza katika vitendo hivyo vya umalaya na uasherati. Daima, mwanaume ndiye huanza kumtongoza mwanamke kushiriki naye ngono. Mwanamke hukubali na ndiyo azma hiyo hufanikiwa. Katika hali ya kawaida yule anayeanza kumshawishi mtu mwingine kufanya jambo baya huwa ndiyo mbaya wa kwanza na nafasi ya pili humwangukia yule aliyeshawishika. Katika hali ya kushangaza, mwanamke ambaye yupo katika nafasi ya kushawishika, ndiye anaonekana kuwa mbaya zaidi kuliko wanaume.

Pia, falsafa juu ya nafasi ya mwanamke inayosawiriwa na Mathias Mnyampala na Shaaban Robert inaonekana kupata mizizi yake katika mafundisho ya dini zao. Shaaban Robert ni Muislamu na Mathias Mnyampala ni Mkiristo. Dini hizi mbili zimetoa mchango mkubwa katika kujenga falsafa yao juu ya mwanamke. Kwa mfano, katika uchambuzi wa data imebainika kuwa mwanamke anapaswa kumnyenyekea mwanaume kwa lugha na maneno mazuri yasiyokuwa ya karaha na matusi. Momanyi (2001) anaunga mkono hoja hii na kusisitiza kwamba, lugha ya matusi haipendezi kwa mtu yoyote na si kwa mwanamke pekee. Hata hivyo, mwanamke kusisitizwa kutokuwa na lugha ya matusi ni kitu cha msingi sana kwa sababu mwanamke ndiye hulea watoto. Hii ni sawa na kusema kuwa, mwanamke hutumia muda wake mwingi kukaa na watoto kuliko mwanaume. Ikitokea mwanamke akawa ni mtu wa kutukanatukana hovyo hovyo iko hatari kubwa kwa

watoto kujifunza lugha ya matusi kutoka kwa mama yao. Falsafa hii ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kumuhusu mwanamke ni muhimu sana katika kuimarisha maadili ya jamii.

Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanaonekana kuwa na falsafa ya kuwaidhi jamii kama njia ya kuleta mabadiliko ya kimaadili kwa wanajamii wote. Mashairi yao mengi yamekaa katika mtindo wa kukataza mambo mabaya na kuamrisha kutendwa kwa mambo mema ndani ya jamii. Ingawa msisitizo wao unaonekana kuilenga jamii nzima lakini kwa kiasi kikubwa mwanamke ndiye anayeonekana kulengwa zaidi na mawaidha yao. Hii inatufanya tuelewe kuwa mabadiliko ya mwanamke kitabia na kimaadili yana mchango mkubwa katika maendeleo ya kitabia na kimaadili ya jamii nzima. Ni sawasawa kabisa na ule msemo wa Waswahili usemao “ukimwelimisha mwanamke umeelimisha jamii nzima.” Msemo huu tumepata kuusema hapo awali na tumeurudia hapa ili kukazia maarifa na uelewa wetu juu ya falsafa walizo nazo Shaaban Robert na Matias Mnyampala juu ya nafasi ya mwanamke ndani ya jamii.

SURA TA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Muhtasari, hitimishi na mapendekezo ya utafiti wote yanatolewa katika sura hii. Muhtasari wa sura zote tano za tasinifu hii utatolewa na kisha kufuatiwa na muhtasari wa madhumuni mahususi ya utafiti. Baada ya hapo kutatolewa hitimishi na mwisho itakuwa ni mapendekezo.

5.1 Muhtasari wa Sura za Tasinifu

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa utafiti ukihusisha vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahususi na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na matatizo ya utafiti na utatuzi wake. Kutokana na vipengele hivi tumeweza kuweka haja ya kufanyika kwa utafiti huu wazi na bayana.

Sura ya pili ya utafiti huu imewasilisha utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kidhamira. Utalii wa kazi tangulizi umefanywa kwa kuanza na kazi zilizofanywa katika kuhakiki mashairi ya Shaaban Robert na kisha kufuatiwa na kazi tangulizi zilizotafiti mashairi ya Mathias Mnyampala. Katika sura hii pia tumewasilisha nadharia ya Ufeministi ambayo ndiyo iliyotumika katika uhakiki wa nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

Sura ya tatu ya utafiti huu imewasilisha njia za utafiti. Njia hizo zimehusisha eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli ya utafiti, mbinu za ukusanyaji wa data; usaili, hojaji na usomaji makini. Vipengele vingine ni mbinu ya uchambuzi wa data ya mkabala

wa kidhamira, kuaminika kwa data za utafiti na usahihi wa data za utafiti zilizokusanywa.

Sura ya nne ya tasinifu hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti. Data hizo zilichambuliwa kwa kufuata mtiririko wa madhumuni mahususi ambapo dhumuni mahususi la kwanza lilihusu kulinganisha na kulinganua nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Mathias Mnyampala na Shaaban Robert. Yaliyowasilishwa kuhusiana na dhumuni hili ni mwanamke kama chombo cha starehe, mwanamke ni mpole na mnyenyekevu, mama na mlezi katika jamii, mwanamke na suala la uaminifu na suala la uasherati na umalaya katika jamii.

Madhumuni mahususi ya pili yalihusu kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha ya kisanaa inayotumiwa kusawiri nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Yaliyobainika katika madhumuni haya ni matumizi ya takriri, matumizi ya tashibiha, matumizi ya taswira na mwisho ni matumizi ya ishara.

Madhumuni mahususi ya tatu ya utafiti huu yalihusu kulinganisha na kulinganua falsafa ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala juu ya mwanamke. Yaliyowasilishwa katika madhumuni mahususi haya ni falsafa ya Shaaban Robert juu ya mwanamke na baadae kufuatiwa na falsafa ya Mathias Mnyampala.

Sura ya tano ya tasinifu hii ndio inayowasilisha muhtasari, hitimishi na mapendekezo yanayohusu utafiti mzima. Katika mtiririko wa sura za tasinifu hii, sura ya tano ndiyo ya mwisho.

5.2 Hitimisho

Hitimisho linalotolewa katika sehemu hii, limezingatia madhumuni ya utafiti ambayo jumla yake yalikuwa matatu.

5.2.1 Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Washairi Teule

Usawiri wa mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume ni dhamira inayoendelea kujitokeza kama dhamira maarufu katika kazi za ushairi za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Shaaban Robert kwa mfano, ametumia lugha ya ishara kuonesha kwamba mwanaume hata akizeeka bado anakuwa na tama ya kufanya ngono za wasichana wadogo. Kimsingi mwanaume huyo hana nguvu za kuweza kufanya tendo la ngono kwa ufanisi lakini kwa sababu anamuona mwanamke kama chombo cha starehe basi anamtamani. Mathias Mnyampala kwa upande wake anamuona mwanamke anayeshiriki katika vitendo vya umalaya na uasherati kuwa anatumia kama chombo cha starehe kwa wanaume. Kama kawaida yake Mathias Mnyampala anatoa waadhi kwa watu kujiepusha na vitendo hivyo kupitia shairi la “Malaya” lililopo katika *Waadhi wa Ushairi*.

Washairi wote wawili wanaonesha kuwa mwanamke ni kiumbe anayetakiwa mpole na mnyenyekevu kwa mume. Unyenyekevu wake utaonekana katika lugha anayoitumia anapoongea na mume wake. Hapaswi kutumia lugha ya matusi wala kujibizana na mume wake. Ngonjera ya “Mke kumba ruhusa kwa Mume” ni mfano mzuri unaonesha maonyo kwa mke kufanya mabishano na mumewe. Hata hivyo, ngonjera hii inaonesha wanawake kuanza kuruka viunzi vya mfumo dume na kuanza kubishana kwa baadhi ya mambo na waume wao.

Mwanamke anasawiriwa kuwa na nafasi kubwa katika malezi ya watoto kutokana na kukaa nao kwa muda mrefu katika siku kuliko ilivyo kwa wanaume. Kwa nafasi hiyo mwanamke hapaswi kutumia lugha ya matusi kwani ni rahisi kwa watoto kuiga lugha hiyo kutoka kwa mama yao. Washairi wote wawili wanaonesha kuwa mwanamke huelemewa na mzigo wa kulea watoto wengi na wakati huo huo akishughulika kwa shughuli nyingine za nyumbani. Wito unaotolewa na washairi hawa kwa wanaume ni kuwa wanaume nao washiriki katika kulea watoto na wasiwaachie wanawake peke yao.

Suala la uasherati na umalaya limeonekana kusukumiwa kwa mwanamke peke yake hali ya kuwa wote wawili hushiriki katika tendo hilo. Shaaban Robert anaonekana kumsawiri mwanamke kuwa ni kinara wa umalaya na uasherati. Mathias Mnyampala anaonekana kuwalaumu wanawake na wanaume kuwa wote ni wahanga wa umalaya na uasherati. Mwanaume ndiye anaanza kumtongoza mwanamke na mwanamke akikubali ndiyo tendo la ngono hufanyika. Kama mwanaume akinyamaza kimya bila ya kutongoza wanawake umalaya na uasherati hautakuwepo katika jamii.

5.2.2 Matumizi ya lugha ya Kisanaa katika Mashairi ya Washairi Teule

Matumizi ya lugha ya kisanaa yanayojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ni mengi nasi tumeteua manne tu. Matumizi hayo ni yale ya takiriri, tashibiha, taswira na ishara. Mbinu hizi za kisanaa kwa ujumla wake zimetumika kutoa msisitizo wa mambo ya msingi ambayo watunzi wapenda jamii iyapate. Kwa mfano, tumeona katika shairi la “Mama” neno “mama” limerudiwa mara nane ili kuonesha kuwa mama ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendeleo yake kwa jumla. Tashibiha zilizotumika katika kazi za Shaaban Robert na

Mathias Mnyampala zinamsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye ana uwezo mkubwa wa kuweza kumfanya mwanaume akaishi au asiishi kwa furaha duniani. Mwanamke huweza kutibua saikolojia ya mwanaume na kumfanya kuwa na mawazo yenye kutafuna mwili wake na kumkondesha. Ushauri unaotolewa na washairi hawa ni kuwa ni lazima mwanaume ampende mkewe kwa dhati ili naye apendwe na mkewe. Hii itawafanya kujaliana na kupendana na kutosababishiana matatizo ya kisaikolojia.

5.2.3 Falsafa ya Washairi Wateule juu ya Mwanamke

Washairi wote wawili wanafalsafa juu ya mwanamke inayokaribiana na kufanana sana kuliko inavyotafautiana. Wanamuona mwanamke kuwa ni kiumbe mwenye nafasi ya juu katika kuleta ustawi wa familia na jamii. Mwanamke ndiye anayeandaa kizazi na taifa la kesho. Ikitokea mwanamke akapata elimu ya kutosha huwa vema katika kuwalea watoto kwa kuwamegea sehemu ya elimu yake na kuwafanya kuwa vijana wenye maadili.

Kwa upande mwingine bado wanaonekana kumsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu ambaye huingia katika maovu kwa vishawishi vya wanaume. Kutokana na hili, mwanamke anaonekana kuwa yeye ndiyo chanzo cha matatizo mengi yakiwamo maradhi katika jamii. Mtazamo huu unajitokeza zaidi katika mashairi ya Shaaban Robert kuliko katika mashairi ya Mathias Mnyampala. Mnyampala anaonesha kwamba, mwanaume na mwanamke wote kwa pamoja wana nafasi sawa katika kuleta maasi na maovu katika jamii. Maovu kama ya zinaa hayafanywi na mtu mmoja bali wote wawili. Mwanaume anaweza akalaumiwa zaidi kwa sababu mara

nyingi yeye amekuwa ndiyo muanzilishi wa maovu hayo kwa kumtongoza mwanamke.

5.3 Mapendekezo

Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wameandika vitabu vingi vya mashairi vinavyoeleza nafasi ya mwanamke katika jamii. Katika utafiti huu tumeteua sehemu tu ya vitabu hivyo visivyofikia nusu ya vitabu vyo. Itakuwa vema kama watafiti wengine nao watachunguza nafasi ya mwanamke katika vitabu vingine vya ushairi vya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

Watafiti wajao wanaweza wakatafiti kwa kina zaidi matumizi ya lugha ya kisanaa inavyotumika katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Sisi tulifanya matumizi ya lugha ya kitamathali kuwa ni moja kati ya mathumuni mahususi ya utafiti wetu. Watafiti wajao wanaweza kulifanya hili kuwa lengo kuu katika utafiti wao.

Ingawa Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ni watunzi wa mashairi ya kimapokeo lakini wanatafautiana katika vipengele kadhaa vya kifani katika utunzi wao wa mashairi. Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kubainisha namna Shaaban Robert wanavyofanana na kutofautiana katika matumizi ya vipengele vya kifani katika mashairi yao. Mathalani, Mathias Mnyampala ana matumizi ya mtindo wa ngonjera katika mashairi yake. Je, Shaaban Robert naye ana matumizi ya mtindo kama huo? Utafiti zaidi ufanyike.

MAREJELEO

Abdullazizi, M.H. (1969), "Ukumbusho wa Marehemu Shehe Shaaban Robert Mathias E. Mnyampala," katika *Kiswahili*. Namba 39, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 2-4.

Babbie, E (1992) *The Practice of Social Research*. 6th edition. Wadsworth Publishing Company.

Best and Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Borg, W.R and Gall, M.D, (2003).*Educational Research: An Introduction***.** Longman London.

Chuachua, R., (2011), *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TATAKI.

Cohen, na Wenzake, (2000) *Research Methods in Education*. 5th edition. London: Rutledge Falmer.

Frolova, N. (2003). "Euphrase Kezilahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry". In *Kiswahili*, Vol. 66 Dar es salaam. IKR.

Inyani, S.K. (2002). *Utafiti wa Kiswahili na Maswala ya Uana: Utafiti wa Kiswahili*. Nairobi. Downtown Printing Works ltd.

Creswell, J.W., (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitatie, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

John, L., (2007), *Critical Reading: A Guide.* In http://www. Brocku. Ca/English/jlge/criticalreadig. Html. Accesssed, 30th, October 2006.

Kezilahabi, E. (1976a), Ushairi wa Shaaban Robert. Nairobi. EALB.

Kezilahabi, E. (1976b), "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya," Tasinifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1983), "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili," katika Makala ya Semina za Kimataifa za Kiswahili namba 3. Dar es Salaam: TUKI.

Khalifa, A.I.S. (2012), "Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania", Dar es Salaam. Tasnifu ya *M.A. Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Khatibu, M.S. (1985), "*Utenzi wa Mwanakupona*," katika, *Mulika* namba 17, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 46-52.

Kihore, Y. M. (1978), "Waadhi wa Ushairi," katika *Mulika*, Namba. 12. Dar es Salaam: TUKI. Kur, 54-59.

Koda, B. (2000) "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District", Unpublished *Ph.D Thesis*, UDSM.

Kothari, R.C. (2009) *Research Methodology. Methods and Techniques* New Delhi: New Age International (P) Limited, Publishers.

Lyatuu, J. (2011), "Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule," Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Macknnon, C.A. (1991), *Toward A Feminist Theory of State*. London: Havard University Pess.

Maganga, M.A (1971), "Maisha ya Shaaban Robert na Mawazo yake," katika Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Nairobi: OUP, pp. 33-54.

Massamba, D. P. B. (1983), "Suala la Ushairi wa Kiswahili," Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili-Fasihi namba 3. Dar es Salaam: TUKI.

Mnyampala, E. M. (1965), *Waadhi wa Ushairi*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Mnyampala, E.M. (1970), *Ngonjera za UKUTA: Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: OUP.

Momanyi, C. (2001), Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi: *Kioo cha lugha.* Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Momanyi, C. (2007), Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry. The Journal of Pan African Studies, Vol.1, no. 8.

Moore, H. (1998), *Feminism and Anthropology*. Mimepolis: University Press of Minnesota.

Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Ndulute, C.L (1985), Politics in Poetic Garb: The Literary Fortunes of Mathias Mnyampala," in Kiswahili, Vol. 52/1&2, Dar es Salaam: TUKI, PP 143-160.

Ndulute, C.L. (1987), "Shaaban Robert's Poetic Land Scape: From Ethinicism to Nationalism," in *Kiswahili,* Vol. 54. Dar es Salaam: TUKI, pp 110-125.

Ndulute, C.L. (1994), *The Poetry of Shaaban Robert*. DUP: Dar es Salaam.

Ngaiza, M.K. (2002), "Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study." Unpublished, *Ph.D. Thesis*, UDSM.

Ngaiza, M.K. (2004), "Harmonization and Mainstreaming Gender in Local Government or Transforming Patriarchy: The Case of Two Wards in Bukoba District Council, Tanzania," In: *Tanzania Journal of Development Studies*, Vol. 5, No. 3 page 25-38.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Ramadhani, S. K. (2013), "Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee". Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Robert, S. (1948), *Pambo la Lugha*. London: Nelson.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*. London: Nelson.

Robert, S. (1967), Kufikirika. Nairobi: OUP.

Robert, S. (1968), *Ashiki Kitabu Hiki*. London: OUP.

Robert, S. (1968), *Kilelezo cha Fasili*. London: Nelson.

Robert, S. (1969), *Mwafrika Aimba*. London: Nelson.

Robert, S. (1971), *Insha na Mashairi*. London: Nelson.

Robson, C., (2007), *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Sengo, T.S.Y., (1975), *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake*, Nairobi: Foundation Books.

Senkoro, F.E.M.K (1968), "Mwamko wa Kisiasa katika Ushairi wa Shaaban Robert," Katika Mulika, Namba 8, Kur. 26- 36.

Senkoro, F.E.M.K (1988), *Ushairi: Natharia na Tahakiki*. DUP: Dar es Salaam.

Shao, I.F. (2004), "Context for Gender Mainstreaming Internationally, Regionally and Nationally," Paper Presented at a Gender Sensitization Workshop for UDSM Council Members, Zanzibar.

Taib, A.H., (2009), "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi," katika Mulika, kur. 130-147. TUKI.

Taib, A.H., (2009), "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi," katika Mulika, kur. 130-147. TUKI.

Wafula, R. M na Njogu, K (2007), Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: The Jomo Kenyatta foundation.

Walibora, K.W. (2013), "Ujasiri wa Kujimulika katika Uandishi wa Kiswahili: Uhakiki wa *Mbali na Nyumbani*," Tawasifu ya Shafi Adam Shafi.

Wamitila, K.W., (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Young, P.V., (1984), *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

Yin, R.K., (1994), *Case Study Research: Design ad Methods*, (2nd eds. Thousands Oaks Calif: SAGE publishers.

VIAMBATANISHO

Kiambatisho A

Dodoso la Usaili wa Ndugu Jamaa na Marafiki wa Shaaban Robert na Mathias Mnyampala

Ninaitwa Ally Edris mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya Mashairi ya Shaaban Robert na hivyo ninaomba ushirikiano wako katika kukamilisha utafiti wangu. Ninayo maswali machache ambayo ninataka kukuuliza huku nikitanguliza shukurani zangu za dhati kwako.

Maswali ya Kudodosa

Sehemu A: Maswali juu ya Shaaban Robert

1. Ninaomba unieleze namna unavyomfahamu Shaaban Robert.
2. Shaaban Robert alikuwa na mahusiano gani na mabinti na wanawake kwa ujumla?
3. Shaaban Robert alipenda kuona mwanamke anapata au anapatiwa nini katika maisha?
4. Umekwishawahi kusoma kazi yoyote ya mashairi ya Shaaban Robert?
5. Shaaban Robert anaeleza nini katika mashairi hayo?
6. Ni upi mtazamo na falsafa ya Shaaban Robert juu ya nafasi ya mwanamke katika jamii?
7. Ni mambo gani yaliyomfanya Shaaban Robert kumsawiri mwanamke hivyo alivyomsawiri katika mashairi yake.

Sehemu B: Maswali kwa Ndugu na Jamaa wa Mathias Mnyampala

8. Ninaomba unieleze namna unavyomfahamu Mathias Mnyampala.
9. Mathias Mnyampala alikuwa na mahusiano gani na mabinti na wanawake kwa ujumla?
10. Mathias Mnyampala alipenda kuona mwanamke anapata au anapatiwa nini katika maisha?
11. Umekwishawahi kusoma kazi yoyote ya mashairi ya Mathias Mnyampala?
12. Mathias Mnyampala anaeleza nini katika mashairi hayo?
13. Ni upi mtazamo na falsafa ya Mathias Mnyampala juu ya nafasi ya mwanamke katika jamii?
14. Ni mambo gani yaliyomfanya Mathias Mnyampala kumsawiri mwanamke hivyo alivyomsawiri katika mashairi yake.

Ninakushukuru Sana

Kiambatanisho B

Hojaji kwa Waliotafiti Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala

Ninaitwa Ally Edris mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya Mashairi ya Shaaban Robert na hivyo ninaomba ushirikiano wako katika kukamilisha utafiti wangu. Ninayo maswali machache ambayo ninataka kukuuliza huku nikitanguliza shukurani zangu za dhati kwako.

Maswali ya Kuhoji

Sehemu A: Maswali juu ya Shaaban Robert

1. Taja kazi za Mashairi ya Shaaban Robert ambazo umezisoma……
   ……
   ……
   ……
   ……
2. Kazi ipi ya Ushairi ambayo imekuvutia sana na kwa nini?
   ……
   ……
   ……
   ……
   ……
3. Shaaban Robert amempa mwanamke nafasi gani katika mashairi yake……
   ……
   ……
   ……
   ……
4. Unafikiri ni kwa nini amempa nafasi hiyo aliyompa……
   ……
   ……
   ……
   ……
   ……
5. Nini Falsafa ya Shaaban Robert juu ya mwanamke katika jamii?.....
   .....
   .....

.....
.....
.....

Sehemu B: Maswali juu ya Mathias Mnyampala

1. Taja kazi za Mashairi ya Mathias Mnyampala ambazo umezisoma……
   ……
   ……
   ……
   ……
2. Kazi ipi ya Ushairi ambayo imekuvutia sana na kwa nini?
   ……
   ……
   ……
   ……
3. Mathias Mnyampala amempa mwanamke nafasi gani katika mashairi yake……
   ……
   ……
   ……
   ……
4. Unafikiri ni kwa nini amempa nafasi hiyo aliyompa……
   ……
   ……
   ……
   ……
   ……
5. Nini Falsafa ya Mathias Mnyampala juu ya mwanamke katika jamii?.....
   .....
   .....
   .....

Ninakushukuru Sana